**28 JUNI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Hamsini na Saba – Tarehe 28 Juni, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi sasa aulize swali lake.

Na. 748

### Hatma ya waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero

**MHE. DENNIS L. LONDO** aliuliza: -

Je, nini hatma ya madai ya maslahi ya waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Jimbo la Mikumi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii zinaonesha kuwa hakuna madai ya mafao ya malimbikizo ambayo yapo kwa waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero. Wafanyakazi wote waliofungua madai wamelipwa. Iwapo kuna mfanyakazi yeyote ambaye hajafungua madai, ninashauri afungue madai yake ili aweze kulipwa mafao yake kwa mujibu wa sheria na kanuni za mifuko zilizopo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, madai ya watumishi wa kilichokuwa Kiwanda cha Sukari Kilombero na *process* nzima ya ubinafsishaji limebaki kuwa kovu kwenye kidonda kwa wananchi hawa.

Swali langu kwa Serikali; kuna mkataba wa hiari kati ya watumishi hawa na kilichokuwa Kiwanda cha Sukari Kilombero ambao haujatekelezwa mpaka sasa; je, nini hatua za Serikali katika utekelezaji wa hilo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna kauli ya Serikali ambayo ilitolewa na Waziri Kusila pamoja na Waziri Kimiti walipokutana na watumishi hawa mwaka 2000.

Nini utekelezaji wake ili kutibu majeraha ambayo yametokana na ubinafsishaji wa kiwanda hiki cha sukari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Londo, hilo la pili Mheshimiwa Naibu Waziri anajua kweli ama unazo hizo taarifa hapa?

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, suala hili lipo katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

**SPIKA:** Hilo ni la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, ni la nyongeza, ndiyo.

**SPIKA:** Ndiyo, sasa ili yeye aweze kuwa na majibu lazima ajue hao wawili uliowataja walisema nini, ndiyo nauliza Mheshimiwa Waziri hizo taarifa za walichosema anazo? Maana swali lako ni la msingi, lakini sasa nataka kujua yeye anayo? Maana asije akatupa majibu ambayo wale hawakusema.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kuwapatia mshahara wa miezi kumi kati ya 40 ambayo ilikuwa ni kifuta jasho kwa watumishi hawa. Sasa utekelezaji mpaka leo hawajatekeleza, nini kauli ya Serikali.

**SPIKA:** Ahaa, kwa hiyo hicho ndicho walischosema hao wawili?

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Jimbo la Mikumi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kuhusiana na mkataba wa hiari aliousema, unaitwa mkataba wa hali bora kwa mujibu wa sheria. Katika mkataba huu wa hiari, bado ni sawa na mikataba mingine kwa mujibu wa Sheria yetu ya Mikataba *Cap. 345,* na kama kutakuwa kuna utekelezaji ambao haukufanyika, hilo ni eneo la kwenda kufuatilia na kuweza kushughulikia.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, mtakumbuka kwamba katika kesi hii ilikuwa ni suala ambalo lilihitaji majadiliano katika upande wa wafanyakazi, Chama cha Waajiri, lakini pia uongozi wa kiwanda wakati wanabinafsisha kiwanda hicho. Na katika kipindi hicho mbali na yale ambayo yalizungumzwa kama utatuzi ya mgogoro, kulikuwa kuna mashauri ambayo yalikwenda mahakamani, sasa katika mashauri yaliyokwenda mahakamani kuna uamuzi wa mahakama ambao ulifanyika, kama malipo yatakuwa hayajafanyika, utaratibu wa kisheria ni kufanya *execution of decree*. Kwa hiyo *enforcement of the execution of decree* kama haikufanyika, nitawasiliana na Mheshimiwa Mbunge tuweze kuona, kwa sababu mahakama ilifanya maamuzi mahususi, niwasiliane naye, na kama kesi hiyo itakuwa kubwa kwa kiwango chake tutaona namna ya kwenda kushirikiana na kukutana na wafanyakazi hao ili haki yao iweze kupatikana kwa mujibu wa sheria na maamuzi ya mahakama, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Mheshimiwa Mbunge.

Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Jaqueline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 749

**Kuweka Vifaa Tiba katika Zahanati Mpya**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kabla zahanati haijafunguliwa inawekewa vifaa tiba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Serikali imetenga shilingi bilioni 15.15 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwenye zahanati ambazo zimekamilika ambapo tayari Serikali imekwishatoa fedha shilingi bilioni 12.90.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 Serikali imetenga fedha shilingi bilioni 18.4 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwenye zahanati zote zinazoendelea kukamilishwa na itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya zahanati zinazoendelea kukamilishwa kwa kadri fedha zinavyopatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaqueline Kainja Andrea, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza; kwa nini Serikali inapotenga pesa za majengo ya zahanati na vituo vya afya isitenge sambamba na pesa za vifaa? Kwa sababu mara nyingi majengo yanafunguliwa wakati vifaa hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; nini tamko la Serikali kwa majibu mazuri yaliyojibiwa hapa kwamba kuna pesa zimetengwa

kwa ajili ya vifaa, tamko la Serikali katika Mkoa wetu wa Tabora kwa zahanati ambazo hazina vifaa na tayari wananchi wanachangishwa pesa za mabenchi kama Zahanati ya Goweko, Kalangale, Wilaya ya Uyui lakini vilevile Wilaya ya Igunga, Kagongo, Kata ya Itunduru na Ibuta - Kata ya Mbutu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, la kwanza, kwa nini Serikali isitenge fedha ya vifaa tiba kwanza; kimekuwa ni kipaumbele cha Serikali kujenga miundombinu kwanza ili huduma zile za msingi ziweze kuanza kutolewa na baada ya kuwa majengo yale yamekamilika na huduma za msingi kuanza kutolewa, ndipo Serikali inatenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na kuvipeleka kwenye zahanati hizo.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilisema kwenye majibu yangu ya msingi, katika mwaka huu wa fedha ambao tunaumaliza, Serikali ilitenga shilingi bilioni 15 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba ambapo tayari bilioni 12.90 imeshanunua vifaa tiba hivyo na vimeanza kusambazwa katika zahanati zote nchini.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili; tamko la Serikali kwa zahanati kupata vifaa tiba katika Mkoa wa Tabora anaotoka Mheshimiwa Mbunge, Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka kipaumbele katika kuhakikisha vifaa tiba vinakuwa katika zahanati zote, vituo vyote vya afya vilevile katika hospitali za wilaya kote nchini katika kuhakikisha afya za Watanzania zinaboreka.

Mheshimiwa Spika, na kwa ajili ya kutekeleza hilo, Serikali imetenga shilingi bilioni 112 kwenye mwaka wa fedha 2023/2024 na vifaa tiba hivyo vitaanza kununulia mara moja mwaka wa fedha unapoanza, na tutaanza kuvisambaza katika maeneo yote nchini

ya zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya, yakiwemo maeneo yale ambayo ameyataja Mheshimiwa Jaqueline Kainja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; je, ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba katika zahanati za Wilaya ya Lushoto zilizokamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali itapeleka vifaa tiba kwenye zahanati za Wilaya ya Lushoto pale ambapo tutaanza utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha wa 2023/2024 ambapo Serikali imetenga shilingi bilioni 112 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kote nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Jaqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 750

**Elimu kuhusu hewa ya ukaa**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kuhusu hewa ya ukaa ili wananchi waelewe na wanufaike na elimu hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, biashara ya kaboni (biashara ya hewa ukaa) ni moja ya mbinu za kupunguza uzalishaji wa gesijoto *(mitigation)* ambayo iliridhiwa katika Itifaki ya Kyoto ikizitaka nchi wanachama kupunguza uzalishaji wa gesijoto iliyorundikana angani. Biashara hii ipo katika masoko ya aina mbili ambayo ni Soko la Hiari/Huria *(Voluntary Carbon Market)* na Soko la Umoja wa Mataifa *(Official Carbon Market)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa Mwongozo wa Biashara ya Kaboni pamoja na Kanuni zake za mwaka 2022. Aidha, elimu kuhusu biashara ya kaboni hadi sasa imetolewa kimakundi ikiwemo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Wizara zote za kisekta pamoja na taasisi zake, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya wote, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mkoa na kwa wadau mbalimbali. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kutoa elimu ya mazingira kwa Umma ikiwemo ya biashara ya kaboni.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Serikali kwamba kupitia jitihada hizo wananchi watapata uelewa na kunufaika na biashara ya kaboni. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Serikali ya 2023/2024 imepanga kutoza asilimia 10 ya mapato ya mnufaika ambaye ni mkulima; kwa nini Serikali isisamehe tozo hiyo kwa wakulima wadogo ili kuwavutia wakulima hao kwenye kuwekeza zaidi kwenye uvunaji wa *carbon*?

Swali la pili, Mwongozo wa *Carbon* wa mwaka 2022 umejikita zaidi katika biashara za *carbon* za misitu mikubwa, lakini Serikali haimtambui mkulima huyu mdogo; je, Serikali itaboresha lini mwongozo huo ili biashara ya *carbon* kwa wakulima itambulike rasmi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia na swali la kwanza; suala la uwepo wa tozo ni suala ambalo lipo kisheria, lakini jambo la kusamehewa tozo ama kupunguza hiyo tozo pia lipo kisheria. Mimi nimwombe tu Mheshimiwa kwamba atupe muda twende tukakae na Wizara inayohusika, wakiwemo wenzetu Wizara ya Fedha, tuone namna ya kuweza kuzungumza nao ili lengo na madhumuni kuweza kuwapa nafasi wakulima wadogo wakaweza ku-*invest* zaidi kwenye *carbon* baada ya kupunguziwa tozo hiyo, kwa sababu biashara hii inalenga zaidi kule kwenye *community*.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, juhudi ya kwanza ambayo tumeifanya ni kutengeneza kanuni na miongozo, jambo ambalo limeshakamilika. Lakini ni kweli tumeona na tumegundua kwamba kuna baadhi ya mapungufu, na sasa hivi ninavyozungumza tumeshaanza kuzifanyia *review* kanuni hizi. Hivi ninavyozungumza kuna timu yetu ipo Morogoro imekaa kwa ajili ya kufanya baadhi ya mapendekezo kuongeza vitu ili mradi tuweze kuwapa nafasi wakulima na wengine.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge baada ya *review* hii tutaona maboresho makubwa yatakayokuja kugusa kwenye sekta za wakulima, sekta za wafugaji na sekta za wafanyabiashara. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Mheshimiwa Mbunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, sasa aulize swali lake.

Na. 751

**Tozo za faini kulingana na ukubwa wa chombo cha moto**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafanya marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani ili kuweka tozo tofauti kulingana na ukubwa wa chombo cha moto?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge anayejibu yupo wapi?

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kufanya marekebisho na kuiboresha Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 ya mwaka 1973 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002. Kwa sasa Serikali inaendelea kuboresha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani ambao tayari ulishasomwa kwa mara

ya kwanza hapa Bungeni. Pamoja na mambo mengine, mswada huo umezingatia mahitaji ya sasa ikiwa ni pamoja na kuweka viwango tofauti vya tozo kulingana na ukubwa wa chombo cha moto kama Mheshimiwa Mbunge anavyoshauri, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza niishukuru sana Serikali kwa usikivu na kusikia ushauri wetu sisi Wabunge, kama ilivyo kwenye Ibara ya 63(2), nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu; je, Serikali itakuwa tayari wakati wanapokamilisha hiyo rasimu ya sheria kunikaribisha na mimi nitoe maoni yangu moja kwa moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada ambapo utungaji wa sheria unahusisha wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na Kamati yako ya Kudumu ya Bunge, Mheshimiwa Mbunge kwa kweli ataalikwa na atashiriki katika hata hatua za mwanzo hadi sheria itakapokamilika, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; bodaboda maeneo ya vijijini ndiyo chombo kikuu cha usafiri kinachotumika kubeba wagonjwa kuwapeleka hospitali; na ili mgonjwa abebwe kwenye bodaboda inabidi abebwe mishikaki, awepo mtu wa kumshikilia, lakini Sheria ya Usalama Barabarani inazuia jambo hilo.

Nini tamko la Serikali juu ya watu wa vijijini wanaotumia bodaboda kupeleka wagonjwa hospitali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kiukweli ni hatari sana watu kutumia bodaboda kwa utaratibu wa mishikaki, na kwa mujibu wa sheria ni hatari kwa usalama wao na maisha yao, na nikiwa Naibu Waziri kwenye Wizara yenye dhamana ya usalama wa raia na mali zao, siwezi kutoa kauli ya kuhalalisha jambo ambalo linaweza likahatarisha usalama wa maisha wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wetu, kama wanaona bodaboda ni chombo, kwa sababu ina magurudumu mawili, tunaweza tukashauri wakatumia chombo kilicho na magurudumu mawili kama baiskeli kuliko kutumia bodaboda ambayo katika kubadili gia, hawa wawili wote wanaweza wakajikuta wamedondoka na wakaathirika kiafya kinyume cha matarajio ya ndugu yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nishauri tu kwamba tuendelee kuimarisha maeneo yetu na kwa namna ambavyo nchi yetu inazidi kuimarika, bila shaka muda mfupi ujao maeneo mengi yatakuwa na usafiri, kwa mfano magari ya michomko, yapo mpaka vijijini, japo hayaruhusiwi kubeba abiria, lakini tumeyavumilia kwa sababu ya mazingira yale, lakini kwenye boda boda ni hatari, hatuwezi kuruhusu jambo hilo.

**SPIKA:** Kwenye baiskeli ni sawa? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nimesema baiskeli kwa sababu ya mwendo wa baiskeli, lakini kiti cha baiskeli kinabeba mtu mmoja tu. Mwendo wake ni mdogo, anatumia nguvu kazi ya yeye mwenyewe, lakini boda boda ni *machine*, ni *engine* sasa ile ni hatari kwa sababu ya ule mwendo wake na kadharika. Baiskeli kumbeba mgonjwa na ndio usafiri tumekuwa tukiutumia maeneo mengi ya vijijini. Tumetumia baiskeli za kwenda taratibu, lakini hii ya bodaboda ni hatari hata sio kwa mgonjwa hata wazima, tunawashauri wasitumie usafiri huo kama mshikaki.

**SPIKA:** Mimi nilitaka kuelewa tu sehemu ndogo, yaani kwamba kwenye baiskeli yule anayeendesha baiskeli akibeba watu wawili zaidi ni sawa?

**NAIBU WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Hapana, kusudio langu abebe mtu mmoja na kile kiti kina uwezo wa kubeba mtu mmoja. Mwendo wake ndio nilisema kwa sababu ya tahadhari anayoisema Mheshimiwa Mbunge kwamba mgonjwa anatakiwa apate mtu wa kum-*support* kwa mwendo wa pikipiki hilo haliwezekani, lakini kwa baiskeli mwendo ule ni mdogo na familia nyingi zimekuwa zikibeba watu hao kwa baiskeli na wanafika, lakini sio pia mshikaki lakini hata kile kiti hakiwezi kubeba mshikaki.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe sasa aulize swali lake.

Na. 752

**Kuondoa changamoto za biashara mpakani**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza:**-**

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuondoa changamoto za biashara za mpakani hasa utitiri wa tozo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Chande majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kavejuru Felix, Mbunge wa Buhigwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, utozwaji wa kodi ya forodha kwa bidhaa zinazoingia nchini kutoka nje ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki unasimamiwa na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Kodi zinazotozwa kwa bidhaa zinazoingia nchini ni pamoja na Ushuru wa forodha ambayo ni ya Afrika Mashariki; kodi ya *VAT* ambayo hutozwa na kila nchi mwanachama; kodi ya ushuru wa bidhaa ambayo hutozwa kwa baadhi ya bidhaa na tozo ya maendeleo ya reli.

Mheshimiwa Spika, tozo nyingine hutozwa kwa huduma zinazotolewa na taasisi mbalimbali za Serikali zinazohusika na uondoshwaji wa mizigo mipakani ambazo husimamiwa kwa mujibu wa sheria zilizoanzisha taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Serikali imefanya jitihada kubwa ya kupunguza changamoto za biashara nchini hususani kupunguza utitiri wa tozo kutoka tozo 380 hadi tozo 148 katika kipindi cha mwaka 2017/2018 hadi 2020/2021. Hivyo Serikali itaendelea kuondoa changamoto za kufanya biashara nchini ikiwemo sehemu za mipakani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kavejuru Felix swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri uko tayari kuja Kigoma baada ya Bunge hili ili uweze kuongea na wafanyabiashara wa Wilaya zote zinazopakana na nchi ya Congo na Burundi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Felix kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida mtoto hufuata kichogo cha mlezi wake. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais mara nyingi anawasikiliza wafanyabiashara na hata Kariakoo alimtuma na kumwelekeza Mheshimiwa Waziri Mkuu akaenda kusimama kwa zaidi ya masaa sita kusikiliza wafanyabiashara, kwa hiyo na mimi niko tayari kwenda Buhigwe na mipakani kuwasikiliza wafanyabiashara. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Frolent Laurent Kyombo swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mpaka wa Mutukula ambao ni mpaka wa Tanzania na Uganda ndani ya Wilaya ya Misenye ni mpaka ambao kiuchumi unakusanya mapato makubwa, lakini wafanyabiashara wa pale wanakabiliwa na utitiri wa tozo ambazo kama mazingira mazuri ya kiwekwa biashara hiyo itakua…

**SPIKA:** Swali lako.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, ni lini sasa Serikali itaboresha mazingira ya biashara katika mpaka wa Mutukula?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika jitihada za kuweka mazingira mazuri ya kibiashara, kwa hiyo, siyo tu sehemu ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge, sehemu zote ambazo ziko mipakani na ambazo sio za mipakani tutajitahidi kuondoa changamoto hiyo ya biashara. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; tatizo sio tozo peke yake kuna utitiri wa vituo bubu vya ukaguzi wa bidhaa barabarani; je, na hivyo vitaondoka lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kajege kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ndio inawezekana lakini naomba hili tulichukue tulifanyie utafiti tuone kama zipo changamoto hizo ambazo zinakwamisha harakati za biashara tuweze kuzipunguza ama kuziondoa kabisa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; mpaka wa Sirari ni mpaka unaongoza kwa wafanyabiashara wadogo kuuawa na askari polisi wanao kusanya kodi.

Ningependa kujua ni lini sasa Serikali itawaondoa askari polisi ambao wanajihusisha na ukusanyaji kodi wanaosababisha mauaji ya hawa wafanyabiashara wadogo wadogo?

**SPIKA:** Nipo natafakari maneno mazito mazito ya watu kuuawa kama vile ni jambo la kawaida hivi, hebu toa maelezo Mheshimiwa Esther Matiko, unavyosema wanauawa unamaanisha hapa unapozungumza na mimi wameshauawa wangapi katika kipindi gani? Maana wanauawa ni kama vile yaani kila wakati kuna jambo linatokea.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; mpaka wa Sirari ni mpaka ambao unaongoza kwa wafanyabiashara wadogo wadogo wanaofanya biashara kati ya Sirari na Kenya kuuawa na askari polisi, mathalani mwezi wa pili kijana Ng'ondi Mheche aliombwa rushwa na askari polisi

anayeshughulika na ukasanyaji wa kodi kinyume na sheria, rushwa ya shilingi 300,000 akiwa na mifuko mitano ya *cement* na alivyogoma wakawa wanamfukuza wakamuuwa na inajulikana.

**SPIKA:** Haya huyo ameshaeleweka, wa pili?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, sasa *case study* ni nyingi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholous Matiko ngoja, taarifa zetu Rasmi za Bunge lazima zikae sawa siwezi nika…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ukiniambie nilete nitaleta ni zaidi ya vijana watano wa Tarime wameshauawa.

**SPIKA:** Kwa sababu ni tuhuma nzito sana yaani kwamba polisi wanafanya kazi ya kuwaua wafanyabiashara wadogo wadogo, ni neno zito sana, yaani kwamba wanauawa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, kwa kauli ya Serikali walizuia kabisa *task force* na polisi kujihusisha na ukusanyaji wa kodi wakaweka mazingira rafiki.

**SPIKA:** Hoja yangu kwako sijui kama umenielewa?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Nimekuelewa.

**SPIKA:** Swali lako ni la msingi, hoja ya msingi ninayoileta kwako unaposema wafanyabiashara wadogo wadogo wanauawa na polisi, hee yaani ni jambo zito ukilisema Bungeni yaani wanauawa na sisi tunaangalia tu, yaani jambo ambalo linatokea, linatokea wanauawa, wanauawa tu, hapana haiwezekani.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba …

**SPIKA:** Ngoja nikupe nafasi, uliza swali lako hilo la kipengele kingine kwa sababu hapa umeingiza na hoja nyingine tena

aliombwa rushwa ya shilingi 300,000, sisi ushahidi huo hatuna ama wewe unao?

Sasa uliza swali lako bila kutaja hayo mauaji maana namna ulivyosema ni kama jambo kule linatokea la kawaida yaani kama liko kila siku kila mwezi na kitu kama hicho. Kwa hiyo, uliza swali lako bila hiyo hoja ya mauaji.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ni lini mtahakikisha mnaondoa askari polisi kujihusisha na ukusanyaji wa kodi kwenye mipaka? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni lini tutaondoa askari polisi? Askari polisi ni chombo cha usalama, usalama wa mali na usalama wa wananchi. Hatuwezi kuwaondoa sehemu za mipakani, kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutafuatilia nini kinatokea huko katika biashara hiyo ya mipakani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Yahaya Massare Mbunge wa Manyoni Magharibi sasa aulize swali lake.

Na. 753

**Kurejeshwa kwa wananchi shamba la iliyokuwa Kampuni ya *Tanganyika Packers* – Itigi Singida**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza: -

Je, kuna maamuzi mengine baada ya Kamati ya Mawaziri nane kurudisha kwa wananchi wa Itigi shamba la Kampuni ya *Tanganyika Packers?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa David Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shamba la iliyokuwa Kampuni ya *Tanganyika Packers* ni kituo cha kupumzishia mifugo kinachojulikana kwa jina la *Kitaraka Holding Ground*. Shamba hili linamilikiwa na Serikali tangu tarehe 1 Mei, 1955 na linatambulika kwa Na. 35 na Hati ya Kumiliki Ardhi Na. 15467 inayotaja ukubwa wa shamba kuwa ni ekari 45,000 (hekta 18,218.623) kwa ajili ya malisho na kutunzia mifugo *(cattle holding ground)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Mawaziri nane wa kisekta ya kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 haijarudisha kwa wananchi wa Itigi shamba la iliyokuwa Kampuni ya *Tanganyika Packers*. Serikali imeelekeza ifanyike tathmini ya kina ya shamba la Kitaraka ili kubaini hali halisi kwa sasa kwa ajili ya kuwezesha Serikali kufanya uamuzi wa kumaliza mgogoro uliopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini kuna swali nauliza.

Mheshimiwa Spika, wale Mawaziri nane walikuja kufanya nini? Leo tunapokuja kusema kwamba Serikali haikuelekeza, haya kama huo ni mgogoro, je tutautatua lini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; jambo la kwanza kwenye ile Kamati ya Mawaziri nane ambayo ilizunguka maeneo mbalimbali nchini, kila eneo lilikuwa linapelekewa taarifa kuhusiana na mahitaji ya eneo husika, sasa katika shamba la *Kitaraka Holding* maamuzi ya Serikali ambayo Kamati ya Mawaziri nane iliyatoa pale ni kwamba sasa ifanyike tathmini ambapo katika ile tathmini tutajua lile shamba wananchi wameingilia kwa kiwango gani ili sasa tuweze kumega sehemu ya lile eneo kuwakabidhi wananchi na sehemu ya eneo ibaki katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kazi ambayo ilikuwa inaifanya hapo awali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasa hivi kinachofanyika, Kamati ya Mawaziri tulikaa na Mheshimiwa Waziri ikaundwa tume maalum ambayo inafanya hiyo tathmini na baada ya hiyo tathmini kukamilika sisi tutakwenda katika eneo hilo kwenda kutoa maamuzi ya mwisho kwa ajili ya wananchi. Kwa hiyo, hiyo ndio kazi kubwa ambayo imefanyika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jerry William Silaa, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, swali la pili hajajibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Kuhusu nini?

**SPIKA:** Swali la pili la nyongeza hajajibu?

**MHE.YAHAYA O. MASSARE:** Ndio.

**SPIKA:** Umeulizaje?

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, kama ni mgogoro ni lini tunaenda kuutatua huu mgogoro, maana yeye amesema ni mgogoro.

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika, nadhani wakati anajibu la kwanza pengine amesema sio mgogoro. Haya naona Mheshimiwa Waziri, amesimama.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Waziri amesimama. Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya kina na ya ufafanuzi mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni lini jambo hili litakwenda kumalizwa; naomba nimhakikishie Mheshimiwa Yahaya Massare kwamba kimsingi kama alivyoeleza Naibu Waziri, jambo lipo mahala pazuri sana na wananchi wa Jimbo lake watapata kunufaika na hiki ambacho Serikali inakwenda kukifanya.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limechelewa kuamuliwa, lakini ndani ya miezi mitatu hii timu ya wataalam itakuwa imekwishakumaliza na tutakwenda sasa rasmi kabisa kukabidhiana kile ambacho tumekubaliana, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, miezi mitatu kwa maana ya mwezi wa tisa tutarejea hapa kuna Bunge tena, kwa hiyo, naamini hilo litakuwa limeshafanyiwa kazi Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Jerry William Silaa, swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza.

Wananchi wa Mtaa wa Bangulo kwenye Kata ya *Pugu Station* walikuwa na mgogoro na shamba la Kabimita ambao Serikali

iliumaliza kupitia Mawaziri wa Ardhi na Mifugo mwaka 2018 lakini mpaka leo wananchi wamefanya urasimishaji na Kabimita kupitia Wizara ya Mifugo haijakabidhi hati ya eneo hilo.

Je, ni lini sasa Serikali itaenda kukabidhi hati hiyo kwa Kamishina wa Ardhi ili wananchi wa Mtaa wa Bungulo Kata ya *Pugu Station* waweze kukabidhiwa hati yao na kuishi kwa amani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Mheshimiwa Waziri amesimama tena, Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge wa Ukonga ka,a ifuatavyo:-

Ni kweli kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan juu ya kutatua migogoro tayari jambo hili tulikwishafika mwisho na Mheshimiwa Jerry kama ambavyo nimemjibu Mheshimiwa Massare katika swali la awali ni kwamba utaratibu wote ulikwisha kufanyika, wananchi wote ambao wanapaswa kupewa haki wanafahamika nani hatua tu za Kiserikali.

Sasa nitamwelekeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Kamishina wa Ardhi, jambo hili lifike mwisho na hatimaye hati iweze kuwa *surrendered* na wale ambao wanapaswa kunufaika, wanufaike na kama kuna malipo ya *premiums* ambazo wanatakiwa kufanya, wanatakiwa wafanye sawa na Sheria za Ardhi zinavyoelekeza, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Zaytun Seif Swai Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 754

**Kupunguza vifo vya watoto wenye umri kati ya sifuri hadi mwaka mmoja**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza vifo vya watoto wenye umri kati ya sifuri hadi mwaka mmoja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya imeweka mipango ya kupunguza vifo vya watoto wenye umri wa sifuri hadi mwaka mmoja kama ifuatavyo: -

Moja, kuongeza vituo vyenye vyumba maalumu kwa ajili ya kutoa huduma kwa watoto wachanga wenye hali mahututi *(Neonatal Care Unit)* kutoka 18 mwaka 2017 kufikia 175 mwaka 2023.

Pili, kutoa mafunzo kwa watoa huduma juu ya namna ya kutoa huduma jumuishi kwa watoto wachanga na watoto wakubwa *(Integrated Management of Childhood Illness-IMCI)*.

Tatu, kuimarisha huduma za kukinga na kuzuia magonjwa yanayozuilika kwa chanjo kama vile surua, nimonia, kuharisha, donda koo, kifaduro, pepo punda na polio kwa kuongeza utoaji wa chanjo za watoto chini ya mwaka mmoja kufikia kiwango cha zaidi ya asilimia 98 ya utoaji wa chanjo ya *Penta 3.*

Nne, Serikali imeongeza vituo vinavyotoa huduma kwa watoto waliozaliwa wakiwa na uzito pungufu *(Kangaroo Mother Care)* ambapo kwa sasa vituo 72 na Hospitali 175 zinatoa huduma hizi. Aidha, kwa mwaka 2023/2024 Serikali imepanga kuongeza vituo 100 ili kufikia vituo 275 ifikapo mwezi Juni, 2024.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, swali la nyongeza.

**MHE.ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu haya ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 70 ya vifo vya watoto vya chini ya miaka mitano, vinatokea kati ya umri wa miaka sifuri hadi mwaka mmojal; je, Serikali haioni haja sasa kuweka mikakati mahsusi na kuwekeza kwa watoto wa umri huo mwaka sifuri hadi mmoja ili kupunguza vifo hivi?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, katika Mkoa wangu wa Arusha moja ya sababu ambayo inapelekea vifo vya watoto wa chini ya mwaka mmoja ni ukosefu wa mashine za kuhifadhi watoto njiti; je, ni lini Serikali itapeleka vifaa hivi katika Hospitali zote za Mkoa wa Arusha? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge hasa kwa jinsi ambavyo anafanya ziara zake kwenye maeneo magumu hasa kwenye maeneo ya Mkoa wa Arusha yasiyofikika. Ni kweli anajua haya matatizo yapo, lakini umeona tulikotoka na mimi nimtoe tu Mheshimiwa Mbunge wasiwasi kwa sababu Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana katika eneo hili, kwa maana ya kuweka vifaa na mambo mengine na mmeona tulikotoka mambo makubwa kama *CT Scan* tulikuwanazo tatu nchi

nzima lakini leo tuna zaidi ya 50, *MRA* mbili lakini leo tuna zaidi ya 19 kwa maana hili nalo ni dogo.

Mheshimiwa Spika, anachokisema Mheshimiwa Mbunge hapa ni kuongeza hiyo huduma. Kwa mwaka huu sasa tunaenda kujenga mia moja maana yake kwa swali lake la kwanza kwamba hilo la maeneo kufikika, maana yake zinajengwa mia moja, maeneo ya Mkoa wa Arusha ni maeneo ambayo pia hivi vituo 100 vinaenda kujengwa kwenye maeneo ambayo hayana.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni suala la kuweka vifaa vya kusaidia hao watoto ambao wanazaliwa kwa uzito mdogo. Ukijenga vituo mia moja na *equipments* zake zinawekwa kule ndani kwa hiyo hilo tatizo litakwenda kutoka na hakutakuwa na tatizo hilo tena.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, licha ya vifo vya watoto wachanga vilevile kuna tatizo kubwa la wazee kwa sababu hawana uwezo wa kulipa gharama na hata vile vitambulisho vinavyotolewa na Halmashauri wengi wa wazee huwa wanapata usumbufu.

Je, ni lini sasa Serikali itatoa bima za afya kwa ajili ya wazee ili waendelee kupata huduma nzuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, suala hili la wazee kuwa na vitambulisho lakini hawapati huduma limekuwa likitokana na upungufu wa dawa na vifaa tiba ambapo hata Mbunge ni shahidi kwa sasa masuala ya upatikanaji wa dawa kwenye vituo vyetu umeongezeka.

Kwa hiyo, hili sasa limeshatatuliwa kwa asilimia 78 kwenye vituo vyetu na hospitali zetu. Hivyo tutaendelea kuongeza mpaka zifike asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, pili, suala ambalo linaweza likatusaidia sisi kuondokana na hili tatizo moja kwa moja, ni sisi Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwamba ni lazima twende kwenye suala la Muswada wa Bima kwa Wote na ndilo suluhisho la kudumu kwa hilo. Lakini wakati huo kabla hatujafikia kwenye suala la Bima ya Afya kwa Wote kuna utaratibu wa kwamba mtu/mzee anayeshindwa kulipa kabisa na anayepata shida tunaweza tukatumia kwa maana ya kupata barua na mambo mengine, lakini sheria zetu vilevile zinatoa *room* kwa watendaji wetu kuwaaandikia barua na kupata huduma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 755

**Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ya kukusanya ya kutumia *passenger service charge***

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza: -

Je, ni lini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itaruhusiwa kukusanya na kutumia *passenger service charge* kuboresha viwanja vya ndege ?

**SPIKA :** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* imewekewa utaratibu wa kukusanya moja kwa moja ada za kutua na maegesho ya ndege; ada ya usalama *(security fee);* tozo za ukodishaji wa ofisi, karakana, majengo ya kuhifadhia mizigo, migahawa na maduka; tozo za maegesho ya magari, na tozo za mabango. Aidha, Sheria ya Huduma za Viwanja vya Ndege *(The Airport Service Charge Act)* Sura ya 365 inaipa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* jukumu la kukusanya tozo kwa abiria wanaosafiri kupitia viwanja vya ndege *(passenger service charge)* na kuwasilisha Hazina.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazokusanywa na *TRA* kutoka kwa abiria na kuwasilishwa Hazina zinatumika kuendeleza miundombinu ya viwanja vya ndege nchini pamoja na kulipa mishahara ya watumishi, matumizi ya uendeshaji wa *TAA* na kufanya matengenezo ya viwanja. Aidha, Serikali hutoa fedha kila mwaka kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge swali la nyongeza.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, kwa kuwa Bunge lilishazimia Kampuni ya *KADCO* kurejeshwa chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, sasa ni lini Serikali itafanya hivyo kutii Azimio la Bunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sawali la pili, ni lini sasa Serikali itakamilisha mchakato wa sheria kuipa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege

kusimamia kuendeleza viwanja vya ndege nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mwezi Novemba, 2022 Bunge lako tukufu liliazimia *KADCO* kuwepo chini ya viwanja vya ndege nchini. Swali la pili, uanzishwaji wa Sheria ya Viwanja vya Ndege nchini. Ninaomba nijibu yote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Bunge lako tukufu kuazimia kwamba lazima *KADCO* iwe chini ya *TAA*, hatua ambayo Serikali tumefanya mpaka sasa, kwanza tuliielekeza *TAA* kuandaa *draft* kwa maana ya mapendekezo ya sheria, na tayari *draft* hiyo imeshakuja Wizarani na tuliyapitia, kuyaboresha na kuyapeleka kwa Mwanasheria Mkuu ili kupata idhini au kibali. Tayari Mwanasheria Mkuu alishatoa kibali na sasa ipo ngazi ya wataalamu kwa maana ya Makatibu Wakuu.

Mheshimiwa Spika, tunategemea tutaomba kibali kwenye Baraza la Mawaziri ambalo litafanyika mwezi wa saba na hatimaye matarajio ya Wizara mwezi wa tisa sheria hiyo iweze kuwasilishwa hapa Bungeni. Sheria hii itaweka msingi wa viwanja vyote vya ndege nchini kuwa chini ya *TAA*.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna viwanja vya ndege vilivyo chini ya *TANAPA,* kuna viwanja vingine viko chini ya mamlaka nyingine za Serikali. Sasa sheria hii itaweka msingi kwamba viwanja vyote vya Serikali hapa nchini viwe chini ya *TAA*, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 756

**Ujenzi wa barabara ya Bunju – Mabwepande – Kibamba Dar es Salaam**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza: -

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Bunju B – Mabwepande – Kibamba utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Bunju B – Mabwepande – Kibamba yenye urefu wa kilometa 24.4 imeanza na inatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2024. Baada ya kazi ya usanifu kukamilika, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima James Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, majibu yanaonesha kwamba usanifu utakamilika mwezi Machi, 2024. Sasa kwa kuzingatia umuhimu wa hii barabara ina hospitali kubwa ya Mabwepande ambayo kama wagonjwa wakizidiwa pale wanapelekwa *referral* Hospitali ya Mloganzila.

Sasa nataka *commitment* ya Serikali kwamba kwa mwaka ujao wa fedha 2024/2025 kwa sababu usanifu utakuwa umekamilika

je, fedha zitaanza kutengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, kuna barabara ya *Old Bagamayo* ambayo inaanzia Morocco, Mwai Kibaki, Daraja la Mlalakuwa pale, *Kawe Round About* mpaka Afrikana; hii imekuwa ni ahadi ya muda mrefu sana ya upanuzi wa ile barabara, na kuna foleni kubwa sana pale, nataka vilevile kupata *commitment* ya Serikali kuwa ni lini upanuzi wa ile barabara utafanyika ili kupunguza kero ya foleni kwa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba hii barabara ya Bunju B – Mabwepande hadi Kibamba ni barabara muhimu sana na imekuwa ikiulizwa mara kwa mara hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge ambao barabara hiyo inapita kwao akiwemo Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo ambapo wiki iliyopita niliulizwa swali hili.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sio tu tunafanya usanifu wa kujenga barabara kama ya barabara ya kawaida kama alivyosema tunajua kuna hospitali, lakini pia tunajua barabara hii kwa sababu pia kuna Kituo cha Mabasi cha Magufuli kitatumika kwa umakini mkubwa sana itakapojengwa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, barabara hii nataka nimjulishe Mheshimiwa Mbunge si tu kwamba itaishia hapo lakini ita–*save* kama barabara ya mzunguko wa nje kwa Dar es Salaam ambayo itatoka hapo Kinamba – Pugu – Toangoma hadi Kigamboni ndio maana huu muda umekuwa mrefu. Kwa hiyo, hako kaeneo alikouliza ni sehemu tu ya hiyo barabara.

Kwa hiyo, *commitment* ya Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara hii tunaijenga kwa sababu sasa tunajua umuhimu wake ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hizi barabara alizosema za kufanya upanuzi kwa sababu ya misongamano, nimuombe Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara alizozitaja tumeziainisha vizuri sana katika kitabu chetu cha bajeti barabara zote za kupunguza misongamano ikiwa ni pamoja na kupanua. Katika kitabu chetu cha bajeti cha mwaka huu barabara nyingi za Dar es Salaam tutazipanua ambazo zinapatikana katika ukurasa wa 259 – 261 atazikuta hizi barabara zote na nini tunafanya katika mwaka huu huu wa fedha ambao tunauendea wa 2023/2024, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima swali la nyongeza.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA**: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza.

Ni lini Serikali itajenga barabara ya mwendokasi yaani *BRT - 4* ambayo kipande kikubwa kinaanzia Mwenge - Makongo Sekondari, Lugalo Jeshini, *Mbezi Beach,* Tegeta kwa Ndevu, Nyaishozi mpaka Basihaya ambayo pia itaondoa mafuriko yanayoikumba Basihaya kwa kujenga mitaro? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gwajima, Mbunge wa Kawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka nimjulishe Mheshimiwa Mbunge wa Kawe kwamba barabara aliyoitaja iko kwenye *BRT - 4* ambayo itaanzia Maktaba itakuja Mwenge mpaka pale Daraja la Kijazi hiyo itakuwa ni *Lot* ya kwanza; na *Lot* ya pili itaanzia Mwenge – Tegeta mpaka kuja huku *DAWASA*.

Kwa hiyo, tutakuwa na wakandarasi wawili; *lot* ya kwanza ndiyo hiyo na *lot* ya tatu itakuwa ni mkandarasi ambaye atajenga majengo.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tarehe 30 Juni, 2023 siku ya Ijumaa pale *DAWASA* tunakwenda kusaini mikataba hiyo ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo ya *BRT - 4,* ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 757

**Huduma ya maji safi na salama - Kyerwa**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza: -

Je, ni wananchi kiasi gani wa Wilaya ya Kyerwa wamefikiwa na huduma ya maji safi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandishi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 Wilaya ya Kyerwa ina jumla ya wananchi 368,360 ambapo kati yao wananchi 209,965 sawa na asilimia 57 wananufaika na huduma ya maji kupitia skimu 26 za maji zilizopo.

Aidha, katika mwaka fedha 2022/2023 Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji ya Runyinya - Chanya, Nyamiaga – Nyakatera - Kagu, Kimuli - Rwanyango na Chakalisa. Miradi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2023 na kuongeza idadi ya wanufaika kufikia 265,219 sawa na asilimia 72 ya wananchi wa Wilaya ya Kyerwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali itaendelea kuboresha huduma ya maji Wilayani Kyerwa kwa kujenga miradi ya maji mipya ya Kikukuru - Mkunyu, Lubilizi, Businde - Nyakashenye, Bugara pamoja na kukarabati Mradi wa Maji Songembele. Kukamilika kwa miradi hiyo kutawezesha wananchi wote Wilayani Kyerwa kupata huduma ya maji safi, salama na ya kutosheleza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, wakati Serikali ikitumia gharama kutafuta vyanzo vya maji, Kyerwa ina vyanzo ambavyo viko tayari; moja ni Mto Kagera lakini na Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza, ni lini Ziwa Victoria na Mto Kagera vitatumika kuwapatia wananchi maji safi na salama ili itimie asilimia 80 kama maeneo mengine?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, wakati Serikali ikiwa na kaulimbiu ya kumtua mama ndoo hata miradi michache iliyopo ya maji wananchi hutembea umbali mrefu kwenda kufuata vyanzo hivyo vya maji.

Swali langu, ni lini au ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha maji hayo yanapatikana kwenye kaya za watu kama ilivyo maeneo ya mjini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anatropia Theonest kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lini Serikali itatumia Ziwa Victoria? Kwenye bajeti yetu ya mwaka 2023/2024 Mheshimiwa Waziri alisisitiza hapa kwamba Ziwa Victoria ni moja ya chanzo ambacho kitaendelea kutumika kwa sababu tayari tumeanza kukitumia kwa maeneo ya Kyerwa na Kyerwa ni Jimbo ambalo nimekwenda mara tatu mimi mwenyewe na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo, kwa hiyo, ni jimbo ambalo nimelifanyia kazi sana. Lengo ni kuhakikisha kwamba kwenye hili swali lako la pili kwamba lini kuona kwamba maeneo yote yatafanyiwa kazi kupata maji safi? Ndio kazi inayoendelea na ni maagizo ya Mheshimiwa Makamu wa Rais ambaye nilikwenda naye pale Kyerwa lakini na sisi kama Wizara tunaendelea kuyafanyia kazi Jimbo la Kyerwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafsi na mimi niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuishukuru Serikali kwa kutuletea Mradi wa Maji kutoka *Lake Victoria* ni lini sasa Serikali italeta mabomba ili kazi ianze kwa kasi kutokana na shida ya maji tuliyonayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Margaret Sitta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni lini mabomba yatafika? Mwezi wa saba tunatarajia mabomba yawe yamefika kutoka India na tayari kazi zimeshaanza, wakandarasi wa miji 28 tayari wapo kazini.

Nikupongeze kwa ufuatiliaji na nilishakuahidi kwamba tutakwenda pamoja Urambo na kuhakikisha mabomba yanaanza kufanya kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa swali la nyongeza. Kwanza niipongeze Wizara tayari imeanza kutumia Mto Kagera kuwapatia wananchi wa Kyerwa maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali, Mradi wa Maji wa Kata ya Kimuli ambao unapeleka kwenye vijiji vitatu tayari umeanza, lakini mkanadarasi haendi vizuri kwa sababu bado hajalipwa pesa ya *certificate* ya kwanza; je, ni lini Serikali itamlipa mkandarasi huyu ili wananchi wa Kata ya Kimuli waanze kupata maji safi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nipokee pongezi kwa sababu kazi inayofanyika ni kwa sababu ya ufuatiliaji wake makini, na kuhusiana na malipo ya mkadarasi Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Wizara tunaendelea na michakato ya kuona wakandarasi wote tunakwenda kuwalipa kwa sababu ni wengi wako kwenye maandalizi ya malipo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 758

**Kutoa mashine kwa vikundi vya wanawake vya ubanguaji korosho 2022/2023**

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kupitia *SIDO* kutoa mashine ndogo na rahisi kwa vikundi vya wanawake vya ubanguaji korosho Mkoani Mtwara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde majibu

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Korosho imeanza kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha korosho zote zinazozalishwa nchini zinabanguliwa na kuuzwa nje ya nchi zikiwa zimebanguliwa *(kernel)*. Lengo kuu ni kuongeza thamani katika zao, kipato kwa wakulima na ajira kwa vijana na wanawake.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kutekeleza mpango huo Serikali imenunua mashine 100 za kubangua korosho zilizotengenezwa na wajasiriamali walio chini ya mwamvuli wa *SIDO* na kuzigawa kwa vikundi 22; vikundi 15 vya Mkoa wa Mtwara na Lindi vikundi saba ambapo jumla ya wanawake 241 na wanaume 18 wamenufaika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania inaendelea kuhamasisha watengenezaji na wauzaji wa mashine za kubangua korosho ikiwa ni pamoja na *SIDO, CAMARTEC* na *TIRDO* ili kurahisisha upatikanaji wa mashine hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza ajira zaidi kwa wanawake kwa kuwa hawa 241 bado ni wachache katika zao la korosho Mkoani Mtwara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Mkoa wa Mtwara haujapata *block farming* katika zao la korosho; Serikali ina mkakati gani wa kuwatengenezea vijana programu mahsusi katika mnyororo wa thamani kwa zao la korosho ili vijana wa Mtawara waweze kunufaika na *project* za Wizara ya Kilimo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 zaidi ya asilimia 60 ya korosho inayozalishwa ndani iweze kubanguliwa na hivyo kutunza ajira zetu za akina mama na vijana kuliko ilivyo hivi sasa ambavyo ajira nyingi zinasafirishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mkakati huo pia hivi sasa tunatazamia kuanza maandalizi ya ujenzi wa *industrial park* katika eneo la Nanyamba ambako tutajenga viwanda vya ubanguaji wa korosho na zaidi ya tani 300,000 zitabanguliwa na akina mama na vijana hawa wataunganishwa katika mfumo uliyosehemu pia ya ajira yao na kutatua changamoto hiyo ya korosho kutokubanguliwa.

Mheshimiwa Spika, la pili la kuhusu mashamba makubwa ya pamoja, utaratibu huo chini ya Bodi ya Korosho umekwisha kuanza

na umeanza kuwapanga wakulima katika mashamba makubwa na ninaamini kabisa kwamba wakulima wa Mtwara wakiwemo akina mama na vijana watanufaika na mpango huo mkubwa sambamba na mkakati mkubwa wa ujenzi wa miundombinu ya skimu za umwagiliaji katika mabonde ambayo pia tutayaweka maeneo kwa ajili ya umwagiliaji wa kilimo cha korosho na hakika pia kupitia utaratibu huu akina mama na vijana wa Mkoa wa Mtwara watanufaika katika mfumo wa mashamba makubwa ya pamoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa uhitaji wa kuongeza thamani kwenye zao la korosho Mtwara unafanana kabisa na uhitaji wa kuongeza thamani kwenye zao la ndizi Kilimanjaro.

Je Serikali ina mpango gani kuwasaidia wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro mashine hizo za *SIDO* ili waweze kuongeza thamani kwenye zao la ndizi kwa kutengeneza *clips* na vitu vingine vinavyotokana na ndizi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha ya kwamba mazao yetu ya kilimo yanachakatwa ili kuongeza thamani na vilevile kuongeza kipato kwa wazalishaji au wakulima wetu na tupo katika mkakati wa pamoja sisi pamoja na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhakikisha kwamba tunatumia taasisi zetu za ndani kama *CAMARTEC, TIRDO* na *SIDO* kutengeneza mashine ndogo ndogo na ambazo zitakuwa zina bei rahisi ili kuweza kuwafikia wakulima wengi zaidi kuongeza thamani ya mazao haya.

Kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba wakulima pia wa ndizi wa Mkoa wa Kilimanjaro hasa akina mama na wenyewe pia tutawaweka na kuhakikisha kwamba na wenyewe wanafanya kazi ya uchakataji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake. Haya kwa niaba yake Mheshimiwa Issa Mtemvu.

Na. 759

**Kuendeleza kilimo cha minazi nchini**

**MHE. ISSA J. MTEMVU K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza kilimo cha minazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha kilimo cha minazi nchini ambapo imeanzisha shamba lenye ukubwa wa hekta 54 katika Kituo Kidogo cha Utafiti cha Chambezi, Wilaya ya Bagamoyo ili kuzalisha miche iliyo bora ya minazi. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imepanga kuzalisha miche bora 750,000 na kuisambaza kwa wakulima wa zao la minazi ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo na kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeanza mazungumzo na Kampuni ya *Deejay Coconut Farm Private Ltd.* ya nchini India katika mashirikiano ya uzalishaji wa miche ya inayozalisha nazi 250 kwa

mnazi mmoja kulinganisha na minazi ya kawaida inayozalisha nazi 80 kwa mti mmoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kuwa na mkakati mzuri wa kuboresha kilimo cha nazi nchini. Nitaomba niwe na swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam pembezoni kwa maeneo ya Kibamba, Segerea na Ukonga pamekuwa na vikundi vingi vinafanya kilimo cha mbogamboga; je, ni upi mkakati wa Serikali kuwawezesha hawa ili wafanye kilimo bora cha mboga mboga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali hivi sasa imeweka mkazo mkubwa kwenye kuhamasisha kilimo cha mboga mboga na matunda ili kuongeza uzalishaji ambao kwa mwaka uliopita kupitia mazao haya yametuletea fedha za kigeni zaidi ya dola milioni 750 na lengo letu kufikia dola bilioni 1.2 kwa mwaka 2030. Hivyo kwa hivi sasa tunaendelea kuwawezesha wakulima wadogo wadogo kwanza kabisa katika upatikanaji wa *green houses* ambao utasaidia katika uzalishaji mkubwa au vilevile mbegu bora ambayo pia itasaidia katika kuzalisha kwa wingi na sambamba na hilo pia tunatafutia masoko kupitia mwamvuli wa *TAHA* ambao hivi sasa tumeshafungua masoko mengi na wakulima wengi wameanza kuuza mboga mboga na matunda nje ya nchi kupitia mwamvuli huu wa *TAHA*.

Kwa hiyo, kama Serikali pia tutahakikisha masoko ya uhakika yanapatikana ili tuendelee kuhamasisha vijana wengi zaidi kushiriki katika kilimo hiki cha mboga mboga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Katika Wilaya yetu ya Kilwa zao hili la minazi limekuwa likiabiliwa na changamoto ya magonjwa mbalimbali na hivyo kupelekea uzalishaji kushuka na umaskini kuongezeka kwa wazalishaji wa zao hili la minazi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto ya magonjwa ya minazi katika Wilaya ya Kilwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kupitia Kituo cha Utafiti cha Kilimo Mikocheni hivi sasa tunaendelea kufanya utafiti wa kuja na miche bora ambayo itakuwa kinzani ya magonjwa na hasa ugonjwa wa manjano ambao unaathiri sana nazi na kufifisha uzalishaji na kwa hivi sasa tunaendelea na uzalishaji wa mbegu mbili kubwa ya *East African Tall* pamoja na *dwarf* ambazo zenyewe zina ukinzani mkubwa wa magonjwa naamini pia wakulima wa Kilwa watanufaika na mbegu hizi na wataongeza uzalishaji kwa sababu kazi ya utafiti imekwisha kufanyika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante naona swali ameshaliuliza Mheshimiwa aliyetangulia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema ataleta mbegu bora za minazi.

Je, katika uletaji wa mbegu bora za minazi mtaangalia na zile mbegu za asili ambazo zilikuwa ni bora zaidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu *(TPHPA)* pale Arusha tunayo benki ya kutunza vinasaba vya mbegu zikiwepo mbegu za asili, kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba tutayazingatia hayo yote pamoja na mbegu za asili ili mwisho wa siku tuhakikishe kwamba uzalishaji unaongezeka, lakini vilevile tunazitunza mbegu zetu hizi kwa sababu zimekuwa zina manufaa makubwa kwa wakulima wetu kwa miaka mingi kabla hatujaleta mbegu hizi ambazo zinatumika hivi sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza kilimo cha michikichi kwenye Mkoa wa Songwe kwa sababu uoto wa eneo hilo unakubali zao hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba zao la mchikichi linaendelea kulimwa katika maeneo yote ambako tumepima afya ya udongo na inakubali na kwa Mkoa wa Songwe kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema sasa hivi tuko katika uzalishaji wa miche na wenyewe pia tutauweka katika mpango wa kuhakikisha kwamba wakulima wa Songwe wanapata miche ya

michikichi na wanafanya uzalishaji kama katika haya maeneo mengine.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi sasa aulize swali lake.

Na. 760

**Viongozi wa Vyama vya Msingi waliodhulumu wakulima wa kahawa – Mbozi**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawachukulia hatua viongozi wa Vyama vya Msingi waliodhulumu fedha za wakulima wa kahawa Mbozi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Jimbo la Mbozi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya uchunguzi kwa Vyama vya Ushirika 20 vilivyopo Wilayani Mbozi ambapo kati ya hivyo, vyama nane vimekutwa na changamoto mbalimbali ikiwemo wakulima kupunjwa malipo ya mauzo ya kahawa; vyama kutowasilisha makato ya ushuru kwa Halmashauri na watoa huduma; na kampuni ya ununuzi wa kahawa kushindwa kulipa fedha za mauzo ya kahawa.

Mheshimiwa Spika, hatua za stahiki zimechukuliwa kwa viongozi na watendaji waliobainika kuhusika na ubadhirifu uliojitokeza. Hatua hizo ni pamoja na kuondolewa kwa viongozi katika nafasi zao; kufanya uchaguzi wa bodi za mpito; na kampuni ya *Taylorwinch* kulipa kiasi cha shilingi 26,978,094 iliyokuwa inadaiwa

na Chama cha Ushirika cha Isaiso. Vilevile taarifa za uchunguzi kwa Vyama vya Ushirika 20 ziliwasilishwa katika Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Songwe kwa ajili ya mapitio na kuchukua hatua kwenye maeneo yenye viashiria vya rushwa, wizi na ubadhirifu.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri kidogo yanatia moyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza wezi wa kuku, wezi wa ng'ombe na mbuzi wakikamatwa wanafikishwa mahakamani, na kufungwa jela, lakini hawa wa Vyama vya Ushirika wanaambiwa tu warudishe fedha na ndio sababu hili tatizo limeota usugu sana Wilayani Mbozi. *(Makofi)*

Sasa ni lini hawa viongozi watafikishwa mahakamani na kuchukuliwa hatua za kisheria? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Afisa Ushirika ambaye ametajwa kwenye hii tuhuma kwamba alishirikiana na hawa viongozi wa Vyama vya Ushirika nashangaa mpaka sasa hivi bado yuko kazini, sasa ni lini na yeye hatua hii itamchukulia? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya uchunguzi taarifa hii imekabidhiwa kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na vyombo vingine vya kisheria kwa ajili ya kuweza kuchukua hatua na ninavyozungumza hivi sasa tayari zaidi ya shilingi milioni 77.6 zimerejeshwa na baadhi ya viongozi wameondolewa na wengine tumewakabidhi TAKUKURU kwa ajili ya hatua za kijinai.

Mheshimiwa Spika, hivyo kazi yetu ilikuwa uchunguzi tumekamilisha, tunasubiri vyombo vingine vya Serikali na vyenyewe vifanye kazi, lakini tu niseme katika hili tumekuwa tukitoa maelekezo

mbalimbali, hatutamvumilia mtu yeyote ambaye atafanya ubadhirifu katika Vyama vya Ushirika na kuwakosesha wakulima mapato yao, Serikali ipo macho tutachukua hatua na hakuna ambaye atapona. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge taarifa iko pale, vyombo vitafanya kazi yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Afisa Ushirika ambaye yuko chini yetu kwa sababu hii taarifa imeshawasilishwa ili kuendana na uwezo wetu tutachukua hatua stahiki pale ambapo itabainika kupitia taarifa ambayo imewasilishwa kwamba ni mhusika moja kwa moja huyu yuko ndani ya uwezo wetu tutachukua hatua stahiki juu yake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Phillipo Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Kwa kuwa wakulima wa Songwe sasa wana imani kubwa na Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na mwaka huu zao la ufuta limevunja rekodi kwa bei nzuri, lakini yupo mnunuzi mmoja amekuja kule, amewarubuni wakulima na Vyama vya Msingi kwa bei nzuri, lakini baada ya hapo baada ya wiki moja ikaonekana hana hela za kuwalipa wakulima. Jambo hilo limeleta taharuki na tumefanya juhudi juu/chini kwa nia ya kutoa semina kidogo kwa Vyama vya Msingi lakini ametusumbua sana.

Je, Serikali inasemaje juu ya mnunuzi huyu ambaye alikuja kuwarubuni wakulima ili angalau wakulima wawe na imani bado na Mfumo wa Stakabadhi Ghalani kwa sababu mpaka sasa ni usumbufu mkubwa umetokea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mulugo hilo liko mahsusi kwa ajili ya huyo mnunuzi labda kama Waziri anamfahamu huyo mnunuzi, kama hamfahamu itakuwa ngumu kidogo kujibu moja kwa moja kwa sababu linamhusu mnunuzi ambaye ametoa ahadi kununua kwa bei kubwa, halafu hakuweza kulipa. Nafikiri kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri yuko hapa na amesikia atakapomaliza kujibu maswali basi utapata nafasi ya kuonana naye ili afanye

mawasiliano na maafisa wake huko mlimalize hilo wananchi wa Songwe wasiendelee na hiyo changamoto.

MheshimiwaJaphet Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa katika msimu wa mwaka jana ambao unaishia sasa hivi baadhi ya wakulima wa zao la kahawa wanavidai Vyama vya Ushirika vingi tu ambavyo bado havijawalipa. Lipi tamko la Serikali kuhusiana na madai hayo ya wakulima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, biashara ya mazao ni biashara kama biashara nyingine yoyote. Vyama vya Ushirika vyote ambavyo havijafanya malipo kwa wakulima vinapaswa kufanya malipo kwa wakulima kwa wakati ili kumsaidia mkulima huyu aendelee na shughuli zake za kilimo, hivyo natumia jukwaa hili la Bunge lako tukufu kuwataka wale wote ambao hawajafanya malipo kwa wakulima wafanye mara moja ili kuwaruhusu wakulima kuendelea na msimu unaokuja wa kilimo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 761

**Utekelezaji wa waraka wa wanafunzi kurejea shuleni**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, ni wanafunzi wangapi wamerejea shuleni tangu waraka wa kuwaruhusu utolewe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpaka kufikia mwezi Januari, 2023 wanafunzi waliorejea shuleni kuendelea na masomo ya elimu ya sekondari ni 1,907 ambapo waliorudi katika mfumo rasmi ni 562 na waliorejea nje ya mfumo rasmi wa elimu kupitia Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari *(SEQUIP)* ni 1,345.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wanafunzi wa elimu ya msingi; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea kukusanya taarifa za wanafunzi waliorejea shuleni baada ya kukatiza masomo kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza nataka kujua hao wanafunzi 1,907 waliorejea shuleni ni asilimia ngapi ya wanafunzi wote ambao walikatisha masomo na walipaswa warejee shuleni?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, nataka kujua kuna haja gani ya kuwaacha watoto nyumbani kwa kipindi cha miezi takribani

minane tangu wafanye mtihani wa *form four* mpaka akajiunge na *form five,* pale pana muda mrefu; kuna sababu gani ya kuacha huo muda kwa sababu kutoka na matokeo ya sensa inaonesha *drop out* pia zinatokea hapo kwa kiasi kikubwa kwa sababu watoto wanakaa nyumbani muda mrefu, kwa nini muda ule usipunguzwe?

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri swali la kwanza linataka takwimu kwa sababu anauliza ni asilimia ngapi? Kama unayo majibu unaweza kumpa, kama huna uyatayarishe kwa maandishi utampelekea Mheshimiwa Mbunge kwa kadri kanuni zetu zinavyohitaji na sasa nakupa nafasi ya kujibu maswali yote kama unayo majibu ya takwimu, kama huna jibu swali la pili, swali la kwanza utampelekea majibu kwa maandishi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili kama ulivyosema swali la kwanza linahusu takwimu. Naomba Mheshimiwa Mbunge aridhie baada ya kipindi cha maswali hapa Bungeni au baada ya Bunge tuweze kukutana kuweza kukokotoa hii *percentage*.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili anataka kufahamu mkakati wa Serikali juu ya kupunguza muda wa wanafunzi kusubiri kujiunga na kidato cha tano pamoja na vyuo vingine.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna kipindi cha zaidi ya miezi saba baada ya wanafunzi kufanya mtihani wa kidato cha nne ili waweze kujiunga aidha na kidato cha tano au na vyuo vingine vya kati.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tunafanya mambo kadhaa ndio maana muda unakuwa mrefu, baada ya mithani kufanyika mwezi wa 11 zoezi la ukusanyaji wa zile *script* ambazo zimetumika kujibia mitihani huwaga zinakusanywa, lakini baada ya hapo tunakwenda kwenye zoezi la usahihishaji, tukimaliza usahihishaji tunakwenda kwenye zoezi sasa la uteuzi wa wanafunzi,

lakini baadae hufanya maandalizi kwa ajili ya wanafunzi hawa sasa kuwapokea kwenye vituo vyetu vya shule mbalimbali. Kwa hiyo, shughuli ambazo zinafanywa katika kipindi hicho ni hizo.

Mheshimiwa Spika, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge Serikali imejidhatiti na kujipanga kwa dhati kuhakikisha kwamba tunapunguza muda huu ambapo sasa tumeanza utaratibu wa kufanya *e-Marking* kwenda kidato cha nne, tulikuwa tumeanza na darasa la saba kwa mithani ya darasa la saba, lakini sasa tunakwenda na hii mithani ya darasa la nne, tumeanzisha mfumo wa *e-Marking* ambao utapunguza muda wa usahihishaji, lakini eneo la pili katika upanganji vilevile tumeanzisha mfumo ambao unajulikana kama *Management Information System* ambao nao vilevile utapunguza muda wa upangaji au uteuzi ule wa wanafunzi kujiunga katika maeneo mbalimbali.

Kwa hiyo, tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kupunguza muda huo ili tuweze kuufanyia kazi sawasawa. Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri leo nilikuwa siwapi ambao wameuliza maswali sana, lakini naona Mheshimiwa Ritta Kabati umesimama kila swali, haya Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwanza kabisa niipongeze Serikali kwa kuona watoto wengi wamerudi mashuleni, lakini mimi swali langu nilitaka kuuliza; je, Serikali inatoa elimu ya makuzi na malezi kwa hawa watoto ili hili tatizo lisiweze kujitokeza tena katika watoto wengine? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatoa elimu hiyo ya makuzi na malezi, lakini nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge katika rasimu ya mitaala pamoja na sera ambayo tunaendelea nayo hivi sasa, maoni ya wadau mbalimbali yameonesha kwamba kuna uhitaji wa masomo haya ya makuzi na malezi. Kwa hiyo, katika mitaala ijayo mambo haya tunaweza kuyaona kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kweni na majibu kutoka upande wa Serikali. Nilete tangazo nilolonalo hapa mbele ni tangazo linalohusu wageni waliokuja Bungeni siku ya leo.

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira hawa ni Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Mkoa wa Dodoma ambao ni Mabalozi wa Mazingira wanaosaidia watoto walio katika mazingira magumu kurudi shule wakiongozwa na Mwenyekiti wa chama hicho, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 12 wa Mheshimiwa Angeline Mabula ambaye Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Wanachama wa Taasisi Isiyo ya Kiserikali ya *SAMASA* inayohusiana na vijana na watoto, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba ambaye ni Waziri wa Fedha na Mipango kutoka Mkoa wa Iringa na Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Anaye mgeni ambaye ni Ndugu Hannaiya Iloko alimaarufu kama *Official Nai*, huyu ni mwanamuziki, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Kabula Shitobela kutoka Jijini Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Cecilia Paresso ambao wafanyakazi wa Benki ya *KCB* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Michael Kembaki ambao ni familia yake kutoka Jijini Arusha wakiongozwa na Mchungaji Charles Mgana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 25 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Agha Khan kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mhadhiri Mwandamizi, Dkt. Tage Biswalo, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Maimuna Mtanda kutoka Tandahimba, Mtwara, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa George Mwenisongole ambaye ni mfanyakazi wa Benki ya *NMB* kutoka Mbozi Mkoa wa Songwe, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao Wageni watatu wa Mheshimiwa Miraji Mtaturu ambao ni viongozi wa dini na mwananchi kutoka Mererani, Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Kenneth Nollo ambao ni watoto wake kutoka Bahi, Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Amandus Chinguile, kutoka Nachingwea Mkoa wa … eeh! Nachingwea imehamia Ruvuma Katibu wa Bunge, haya kutoka Nachingwea Mkoa wa Lindi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Joseph Kakunda kutoka Sikonge, Mkoa wa Tabora, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wageni watano ambao wanatokea *Mtembezi Adventure* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hilo ndio tangazo nililonalo hapa mbele, tunaendelea na ratiba yetu. Mheshimiwa Kasalali Mageni.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 76; hapo awali nilipata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kuhusu msimamo wa Serikali juu wa utumikaji wa chombo cha usafiri aina ya bodaboda katika kubeba wagonjwa hasa kwenye maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu bodaboda ni chombo ambacho kinatumia magurudumu mawili na mgonjwa anapokuwa anapelekwa hospitali mara nyingi katika hali dhoofu huwa anahitaji kuwa na mtu nyuma wa kumshikilia na katika sheria zetu za usalama barabarani hicho kitendo kinaitwa mshikaki.

Kwa hiyo, nilitaka kufahamu msimamo wa Serikali juu ya kusaidia wagonjwa wetu ambao ni lazima wafanye hivyo ili wakapate huduma za hospitali, lakini katika majibu yake Mheshimiwa Waziri akawa ameshauri tutumie baiskeli ambacho ni

chombo cha kizamani zaidi na kinakwenda polepole zaidi, kwa hiyo, inaondoa ule uharaka na umuhimu wa kumuwaisha mtu hospitali na niliomba msimamo wa Serikali kwa sababu watu wengi wa vijiji chombo ambacho kinaokoa maisha yao kwa sasa wanapougua ni bodaboda, lakini wakiwa wanaenda hospitali wakakutana na polisi inakuwa ni mushkheri na wanapata matatizo makubwa ambayo wakati mwingine inapelekea kucheleweshwa kwa wagonjwa hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kufahamu kama bodaboda hairuhusiwi, lakini baiskeli inaruhusiwa kubeba mshikaki kupeleka mgonjwa hospitali.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Kasalali Mageni akiomba mwongozo kwa swali alililoliuliza kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Swali lake lilikuwa ni swali la nyongeza, lakini swali la msingi lilikuwa la Mbunge mwingine na tulishatoa Mwongozo hapa Bungeni kuhusu nani anaweza kuomba kwamba swali lake lijibiwe kikamilifu; ni yule mwenye swali la msingi, ya nyongeza tunayataraji pia yajibiwe kikamilifu kabisa, lakini kwa sababu ni la nyongeza maana yake sasa Waziri anaweza kuwa hajajipanga kujibu kwenye hilo eneo kwa mawanda yake.

Waheshimiwa Wabunge, lakini hata hivyo kwa sababu jambo hili lililozungumzwa linahusu kuokoa maisha ya wananchi na wakati mwingine yanakuwa ni ya mama mjamzito anapaswa kuwaishwa kwenye kituo cha afya ama zahanati kwenda kujifungua, kwa mazingira hayo nadhani Serikali kipingi hiki imekuwa ikijibu maswali mengi hasa kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhusu magari mengi ya kubebea wagonjwa ambayo yanakuja na ambayo yatapelekwa nadhani majibu yao yameashiria kwamba kila jimbo litapata magari mawili, lakini sisi hapa Bunge tumewashauri kwamba waangalie

namna ambayo majimbo mengine ni madogo, kwa hiyo, kupeleka magari mawili ni kama litakuwa linakaa tu pale. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wao wamechukua huo ushauri na wanaenda kufanya sasa kazi hiyo. Kwa hiyo, naamini hata yale maeneo ambayo hayafikiki kabisa, Serikali itatazama namna ya kupeleka usafiri huo ambao imechukua hatua hizo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wagonjwa wanafika hospitali wakiwa salama.

Sasa kuhusu matumizi ya hiki chombo, Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwa ujumla wake kuhusu mipaka ambayo sheria yetu inaweka kwa ajili ya kuhakikisha raia wenzetu wanakuwa salama. Hayo ni mazingira ya kawaida na ni sheria ndivyo inavyosema, lakini kwa sababu huyo ni katazo la jumla, yule askari anayetaka kumshusha mgonjwa kwenye bodaboda nadhani yeye ndio anashida kuliko sheria, kwa sababu anamuona ni mgonjwa na anataka amshushe ili amfanye nini sasa pale kwa sababu huyu anayeendesha chombo hawezi kumbeba huyo mgonjwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nadhani ni jambo ambalo ni la kutazama katika mazingira ya udharura na kwa namna hiyo kwa sababu sheria yetu inalikataza jambo hilo kwa ujumla Waziri hawezi kutoa agizo hapa kwamba jamani akiwa mgonjwa abebwe, hapana. Ndio maana Serikali inafanya hatua mbalimbali za kuhakikisha wagonjwa wanafikishwa hospitali salama wakiwa kwenye gari ya kubebea wagonjwa, lakini kwa yale mazingira ya udharura nadhani maaskari washauriwe tu na sisi kama Bunge tunawashauri waangalie mazingira ya wale wanaowakamata kwa maana ya kwamba wakiona yule aliyebewa ni mgonjwa wamuache awahi hospitali, kwa sababu hata wakikaa naye pale wao sio madaktari. Kwa hiyo, wamuache awahishwe hospitali na huwezi kukaataa kwa sababu mwingine angebebwa mgongoni. Sasa akibebwa mgongoni ataaenda mwendo gani na akibebwa mgongoni huwezi kumkakamata. Sasa kama akibebwa mgongoni huwezi kumkamata basi hata hicho chombo kinachomsindikiza kama ni mgonjwa kweli basi usimkamate, muache amuwahishe mgonjwa hospitali, lakini hata hivyo natambua unaweza ukawepo udanganyifu kwa maana

ya kwamba mtu sasa kwa sababu amekamatwa anajifanya sasa amezidiwa na homa imepanda nadhani askari watatumia hekima kutazama nani ni mgonjwa na nani sio mgonjwa kuliko kuwakamata wale ambao wamebeba wagonjwa halafu mgonjwa anafia njiani, inakuwa kidogo haileti picha nzuri, kwa sababu ni mazingira ya dharura kwa hiyo lazima utumie njia za dharura. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema maelezo hayo ambayo kimsingi sio mwongozo ambao ameuomba kwa sababu kikanuni mwongozo huo ulipaswa kuombwa na mwenye swali la msingi lakini nimeona nitoe maelezo hayo ya ziada kwa sababu ya mazingira ya vijijini wakati tukisubiri magari ambayo yanaletwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma kwa mwaka 2023**
***(The Public Procurement Bill 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Muswada umesoma kwa mara ya kwanza kwa hiyo tutaupeleka kwenye Kamati ambayo tutaona inaweza kufanya kazi hii kwa ufanisi na kwamba liko chini ya hiyo Kamati.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Muswada huu nao umeshasomwa kwa mara ya kwanza na tutaupeleka kwenye Kamati ambayo itaufanyia kazi.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**SPIKA:** Taarifa ya Katibu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge nimwite sasa Katibu atusomee.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge sasa zimemalizika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndio taarifa ya Katibu wa Bunge.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**SPIKA:** Hoja ya Kuahirisha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge sasa, nimwite Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, aje atoe Hoja ya KUHITIMISHA Bunge. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa fadhila zake ambazo zimetuwezesha hapa leo katika siku hii muhimu sana ambapo tunahitimisha Shughuli za Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulioanza tarehe 4 Aprili, 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge hili kwa hekima na weledi wa hali ya juu. Sote tumeshuhudia umeongoza vyema mijadala ya mkutano huu kwa mustakabali wa maendeleo ya wananchi wa Tanzania kupitia mawasilisho ya Bajeti ya Serikali na sekta zake. Nimpongeze pia Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukusaidia vizuri kuliongoza Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini kwa kuchaguliwa kuendelea kushika nafasi za Mwenyekiti wa Bunge. Aidha, nina mpongeza Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini kwa kuchaguliwa kwa mara ya kwanza na Bunge lako tukufu kuwa Mwenyekiti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hongereni sana kwa kuaminiwa na Waheshimiwa Wabunge kushika nafasi hizo za uongozi. Sote tumeshuhudia mmeendesha vyema mijadala ya Bunge mmeonyesha ustamilivu, hekima na uwezo mkubwa wakati wote mlipokuwa mkisaidia majukumu ya Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kuwasilisha hoja za bajeti za kisekta, kutoa ufafanuzi na kujibu hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mijadala ya hoja hizo. Ni imani yangu kuwa

hoja hizo zitakuwa chachu katika utekelezaji wa mipango ya Serikali iliyowasilishwa kupitia bajetii.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao muhimu yenye lengo la kulinda, kusimamia na kuboresha ustawi wa Watanzania. Hakika mmefanya kazi nzuri ya uwakilishi kwa kuleta hoja zenu zenye nguvu katika kipindi chote cha mkutano huu tangu ulipoanza. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kutekeleza kikamilifu jukumu lenu kwa mujibu wa Katiba wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kupitia, kujadili na kupitisha Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kwa weledi wake na uongozi wake mahiri katika vikao vya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ya mwaka 2023/2024 kwa mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilihakikishie Bunge lako tukufu kuwa Serikali imepokea maoni na michango yote na baada ya kuhitimishwa Mkutano huu itasimamia ipasavyo utekelezaji wa bajeti hii. Aidha, itaimarisha nidhamu na matumizi ya fedha za umma pamoja na kuelekeza fedha kwenye maeneo muhimu ya vipaumbele kama yalivyoainishwa katika bajeti ya mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kukupongeza sana wewe binafsi kwa uthubutu ulionao ikiwemo kuamua kugombea nafasi ya Rais wa Bunge la Dunia. Hatua hiyo imelijengea heshima kubwa Taifa letu, ama kwa hakika unatosha kwa nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kukutakia kila la kheri katika kinyang'anyiro hicho na tunamuomba Mwenyezi Mungu akuwezeshe. Niwasihi sana Watanzania wote tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Spika

na kumuomba Mwenyezi Mungu ili mchakato huo ukawe wa kheri na ushindi *Inshallah* Mwenyezi Mungu atakujaalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Bunge lako tukufu likiendelea na vikao vyake, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya teuzi na mabadiliko ya baadhi ya watendaji wakuu wa taasisi, mabalozi na viongozi wa Tawala za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Nitumie fursa hii kuwapongeza viongozi wote walioteuliwa kushika nyadhifa hizo na kuwatakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yao mapya. Niwasihi sana wateuliwa wote nendeni mkasaidie kutatua kero za wananchi. Hakikisheni mnawapokea, mnawasikiliza na kutafuta suluhu ya changamoto zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa wateuliwa wote wafanye kazi kwa uzalendo, weledi wakitanguliza kwanza maslahi ya Taifa. Matarajio ya Mheshimiwa Rais katika mabadiliko hayo ni kuongeza ufanisi katika utumishi wa umma hivyo kila mmoja katika dhamana aliyopewa ahakikishe anakidhi matamanio hayo na kuacha alama au matokeo chanya katika ofisi anayoitumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe salamu za pole; wakati tukiendelea na Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge lako tukufu, tuliondokewa na wapendwa wetu wanasiasa nguli na Wabunge wastaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tarehe 18 Aprili, 2023 tulimpoteza Mheshimiwa Nimrod Mkono aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Butiama, lakini vilevile tarehe 12 Mei, 2023 tulimpoteza Mwanadiplomasia mashuhuri Mheshimiwa Benard Camillus Membe aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Mtama na Waziri Mstaafu.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kutoa salamu za pole kwa familia, ndugu na jamaa wa marehemu na Watanzania kwa ujumla. Hakika viongozi hao watakumbukwa kwa umahiri wao, busara zao, pamoja na ushawishi mkubwa wa kisiasa ndani ya nje ya nchi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kupumzisha roho zao mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, vilevile nitoe pole kwa Watanzania wote waliopoteza wapendwa wao na wengine kujeruhiwa katika matukio mbalimbali zikiwemo ajali za vyombo vya usafiri. Tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu awajalie majeruhi wote afya njema na aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu wa Bunge, jumla ya maswali 761 ya msingi na mengine 2,581 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Pia jumla ya maswali 17 ya papo kwa papo yalielekezwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na kujibiwa. Maswali hayo ambayo yalihusu sekta mbalimbali yameonesha umahiri wenu katika kufuatilia masuala ya maendeleo katika maeneo yenu pamoja na nchi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mkutano huu Bunge lako tukufu lilipokea na kujadili taarifa mbalimbali za Kamati za Kudumu za Bunge ambazo zilibeba maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ya msingi kwa Serikali, baadhi ya hoja zilizofanyiwa kazi na Serikali wakati wa Mkutano huu wa Bunge ukiendelea. Nitumie fursa hii kulihakikishia Bunge lako tukufu na Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imepokea hoja zote na itaendelea kuzifanyia kazi na mara utekelezaji wake utakapokamilika itatoa mrejesho. Aidha, naziagiza Wizara zote ziendelee kufanyia kazi maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu pia, Bunge lako tukufu limepokea miswada saba ya sheria kama ifuatavyo:-

(i) Muswada wa kwanza ni Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa mwaka 2023 *(The Planning Commission Bill 2023)* umesomwa na hatua zake zote na kupitishwa na Bunge;

(ii) Muswada wa pili ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa mwaka 2023 *(The Tanzania Intelligence and Security Services Amendment Bill 2023)* umesomwa kwa hatua zake zote na kupitishwa na Bunge;

(iii) Muswada wa tatu ni Muswada ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali yatokanayo na Urekebu wa Sheria wa mwaka 2023 *(The Laws Revision Miscellaneous Amendment Bill 2023)* umesomwa kwa hatua zake zote na kupitishwa na Bunge;

(iv) Muswada wa nne ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa mwaka 2023 umesomwa kwa hatua zake zote na kupitishwa na Bunge;

(v) Muswada wa tano ni Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kwa mwaka 2023 *(The Appropriation Bill 2023)* Muswada ambao ulisomwa kwa hatua zake zote na kupitishwa na Bunge;

(vi) Muswada wa sita ni Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2023 *(The Finance Bill 2023)* Muswada ambao ulisomwa na hatua zake zote na kupitishwa na Bunge;

(vii) Muswada wa saba ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment Bill (No. 2) 2023)* umesomwa kwa mara ya kwanza; na

(viii) Nane ni Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma kwa mwaka 2023 *(The Public Procurement Bill 2023)* umesomwa kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 61 na 107 hadi 112 za Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 na kwa kuzingatia wajibu wa Bunge katika kusimamia na kuishauri Serikali, Bunge lako tukufu lilipokea, kujadili na kupitisha maazimio manne kama ifuatavyo:-

(i) Azimio la kwanza ni Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa kuimarisha demokrasia nchini na kukuza diplomasia ya uchumi;

(ii) Azimio la pili ni Azimio la Bunge kuruhusu pendekezo la kuridhiwa makubaliano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kwa lengo la kuanzisha ushirikiano wa kichumi na kijamii katika uendeshaji wa maeneo ya bandari nchini;

(iii) Azimio la tatu ni Azimio la Bunge la kuridhia kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ili kuruhusu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Misitu Kigosi; na

(iv) Azimio la nne ni Azimio la Bunge la kuridhia kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, baada ya kujadili kwa kina walipitisha kwa kishindo maazimio hayo muhimu kwa mustakabali wa ustawi wa maendeleo ya wananchi wa Tanzania. Nitumie fursa hii kulipongeza Bunge lako tukufu kwa uzalendo na uamuzi sahihi wenye nia ya dhati wa kukuza uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kauli za Serikali Bungeni; kwa mujibu wa Kanuni ya 56 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 Bunge lako tukufu katika Mkutano wa Kumi na Moja lilipokea kauli za Serikali zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa Bunge lako tukufu tarehe 19 Aprili, 2023 lilipokea Kauli ya Serikali kuhusu mapigano katika nchi ya Sudan. Kauli hiyo ilitoa mwelekeo wa Tanzania na kuzitaka pande zinazopingana zisitishe mapigano hayo na kufanya mazungumzo ya mezani ili kufikia muafaka.

Vilevile tarehe 15 Mei, 2023 Bunge lako tukufu lilipokea Kauli ya Serikali kuhusu tukio la wananchi watano kujeruhiwa na askari wa

*TANAPA* katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Wilayani Mbarali, Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita leo tunapohitimisha shughuli za Mkutano wa Kumi na Moja ambapo pamoja na mambo mengine Bunge lako tukufu limefanikiwa kupitia, kujadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/2024, bajeti tuliyoipitisha imethibitisha uthubutu alionao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ni Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuwaletea maendeleo Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa kurudia kile kilichokwisha kujadiliwa wakati wote wa mkutano huu kwa kuwa Waheshimiwa Mawaziri walitoa ufafanuzi wa kutosha wa hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge. Hata hivyo, niruhusu nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi sana baadhi ya mambo ambayo yanaakisi dhamira, uthubutu, maono na azma ya Rais wetu wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na hii ni katika kupiga hatua kubwa ya maendeleo ndani ya kipindi kifupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mambo hayo ni kuimarisha huduma za usafiri na usafirishaji ikiwemo ununuzi wa ndege ya mizigo na ujenzi wa viwanja vya ndege, kutoa fidia kwa wananchi walio jirani na migodi ya Liganga na Mchuchuma, kuimarisha upatikanaji wa mawasiliano nchi nzima kwa ujenzi wa minara ya mawasiliano na uzinduzi wa Ikulu ya Chamwino. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na ununuzi wa ndege ya mizigo; Serikali imeendelea kuimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)* kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ili iweze kujiendesha kibiashara. Mikakati iliyotekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 ni pamoja na kununua ndege mpya. Hadi sasa tayari Serikali imepokea ndege moja ya mizigo *Boeing 767 – 300F* ambayo iliwasili nchini tarehe 3 Juni, 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hii ni ya kujivunia kwani ndege hii kubwa yenye uwezo wa kubeba hadi tani 54 za mizigo kwa wakati mmoja itasaidia nchi yetu kuongeza uwezo wa kusafirisha bidhaa za mazao kutoka sehemu mbalimbali nchini kwenda nje ya nchi. Bidhaa hizo ni pamoja na minofu ya samaki, dagaa, samaki wa mapambo, nyama, maua, matunda, mboga mboga na mazao ya baharini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni ulipaji fidia wananchi wa Liganga na Mchuchuma. Utekelezaji wa Mradi wa Liganga na Mchuchuma unajumuisha uchimbaji wa chuma cha Liganga pamoja na makaa ya mawe kule Mchuchuma. Tafiti zilizofanywa tangu mwaka 2013 zilibainisha uwepo wa tani milioni 428 za makaa ya mawe ambazo zinaweza kuchimbwa kwa miaka zaidi ya 140 pamoja na tani za chuma zaidi ya milioni 126 ambazo zinaweza kuchimbwa kwa miaka 58. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya awali Serikali imekamilisha malipo ya fidia kwa wananchi 1,142 waliotoa maeneo yao ili kupisha utekelezaji wa mradi huo wa Liganga na Mchuchuma kule Wilayani Ludewa, Mkoani Njombe ambapo shilingi bilioni 15.4 zimetolewa. Malipo hayo yamejumuisha fidia pamoja na riba ya miaka saba tangu wananchi hao walipofanyiwa tathmini. Ninampongeza sana Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hatua hiyo muhimu aliyoitekeleza. Niwaombe wananchi waendelee kuiunga mkono Serikali katika utekelezaji wa mradi huo muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuimarisha upatikanaji wa mawasiliano ya simu maeneo ya vijijini. Serikali imeendelea kuimarisha huduma za mawasiliano mpaka vijijini. Katika kutekeleza azma hiyo hivi karibuni Serikali imetia saini mikataba ya kupeleka huduma za mawasiliano nchini baina ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* na watoahuduma za mawasiliano nchini. Mikataba hiyo itawezesha kujengwa kwa minara 758 katika kata 713 na hivyo kusaidia kuimarisha mawasiliano katika maeneo hayo na mikataba hiyo ina thamani ya shilingi bilioni 265.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hizo pia zinawezesha mradi wa kuongeza uwezo wa minara 304 ya mawasiliano utakaogharimu shilingi bilioni 10.2. Lengo la mradi huu ni kuongeza nguvu katika minara 304 ambayo awali ilikuwa inatoa huduma ya *2G*. Minara hiyo sasa itaanza kutoa huduma za *3G* na *4G* katika baadhi ya maeneo huko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni uzinduzi wa Ikulu Chamwino; itakumbukwa kuwa tarehe 20 Mei, 2023 tulishuhudia tukio la kihistoria ambapo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Ikulu ya Chamwino. Nitoe pongezi nyingi sana kwake Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kwa hatua hiyo ya kihistoria, uzinduzi wa Ikulu Chamwino ni kielelezo cha utashi na ushupavu wa Rais wetu mpendwa katika kuhakikisha kuwa ustawi na maendeleo ya makao makuu ya nchi yetu unaimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapongeza viongozi wote wa taasisi zote zilizoshiriki kikamilifu katika usimamizi na ujenzi wa Ikulu hiyo ya Chamwino. Kimsingi ujenzi huu ni kielelezo cha nchi yetu kuweza kujisimamia na kujitegemea kwani ni Ikulu iliyojengwa kwa fedha zetu, wataalamu wetu na ndani ya taasisi zetu ni ujenzi ambao umesimamiwa kizalendo na kwa moyo wa kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni ukamilishaji wa majengo ya Ofisi za Serikali kule Mtumba; katika kukamilisha azma ya kuhamia Dodoma Serikali inaendelea na ujenzi wa majengo 29 ya ghorofa katika Mji wa Serikali pale Mtumba. Kati ya majengo hayo 26 ni ya Ofisi ya Wizara na majengo matatu ni ya taasisi. Hadi kufikia tarehe 16 Juni, 2023 jumla ya shilingi bilioni 321 zimetolewa kwa wakandarasi na washauri elekezi kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo hayo. Aidha, ujenzi wa majengo hayo unaendelea sambamba na ujenzi wa miundombinu ya huduma za barabara, maji safi, maji taka, umeme, gesi, mawasiliano, TEHAMA, usalama, zimamoto na uokoaji na utaratibu wa programu za upandaji wa miti. Nitumie fursa hii kuzisisitiza Wizara na taasisi ziharakishe ujenzi ili

kuanzia Januari 2024 majengo hayo mapya yaanze kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa uwanja wa mashujaa pale Mtumba; sambamba na ujenzi wa majengo ya ofisi, Serikali inaendelea na ujenzi wa uwanja wa mashujaa ambapo kutakuwa na mnara wa mashujaa na bustani ya mapumziko katika Mji wa Serikali. Mradi huo unatekelezwa kwa awamu ambapo katika awamu ya kwanza unahusisha ujenzi wa uwanja wa gwaride. Ujenzi wa uwanja wa gwaride unatarajiwa kukamilika mapema ili kuwezesha maazimisho ya Siku ya Mashujaa tarehe 25 Julai, 2023 kufanyika katika uwanja huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni usafiri wa mabasi ya mikoani; itakumbukwa kwamba mwishoni mwa miaka ya 1990 Serikali ilizuia mabasi ya abiria kusafiri usiku. Zuio hilo lilisababishwa na matukio ya utekaji wa mabasi uliohusisha uporaji na udhalilishaji wa abiria, na ajali mbaya za mabasi zilizogharimu maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, sote ni mashahidi kuwa changamoto za usalama na miundombinu zilizokuwepo kipindi hicho zimepungua kwa kiasi kikubwa au kuondolewa kabisa kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Miundombinu hii ya barabara na mawasiliano ya simu vimeimarishwa karibu maeneo yote nchini. Aidha, juhudi za Jeshi la Polisi katika kupambana na kudhibiti uhalifu ikiwemo kufanya doria katika barabara kuu na barabara za mikoa na Mamlaka ya Usimamizi ya Usaifiri wa Nchi Kavu *(LATRA)* kuanza kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji wa mwendokasi wa mabasi ya abiria *(VTS)* vimesaidia sana kupunguza matukio makubwa ya ajali za barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia mabadiliko hayo chanya na maoni ya wadau mbalimbali wa usafiri na usafirishaji wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, utayari wa wamiliki na madereva wa mabasi kuzingatia sheria na kanuni za usalama barabarani na utayari wa Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama

kuimarisha doria Serikali imeamua kuondoa zuio hilo la mabasi ya abiria kusafiri nyakati za usiku lililowekwa miaka ya 1990. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo lilikuwa ni kutekeleza uamuzi huu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itashirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi hususani Sekta ya Uchukuzi kuweka utaratibu utakaofuatwa na wamiliki na madereva wa mabasi ya abiria wenye nia ya kusafiri nyakati hizo ili kufika maeneo walikokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la uboreshaji wa huduma za bandari nchini; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020/2025 inaelekeza kuboresha miundombinu ya bandari na kuondoa urasimu katika utoaji wa mizigo bandarini. Katika kutekeleza azma hiyo Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya bandari ili kuongeza ufanisi, mapato ya Serikali na kutoa huduma bora kwa wananchi na watumiaji wengine wa bandari zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa bandari unaofanywa na Serikali unahusisha bandari zilizopo katika bahari hususani Bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara kukiwa na bandari ndogo za Lindi, Kilwa, Bagamoyo na Pangani. Serikali imefanya maboresho katika Bandari ya Tanga ikiwemo kuchimba lango la kuingilia bandarini na kununua mitambo ya kisasa. Katika Bandari ya Mtwara tumejenga gati jipya na kununua mitambo ya kisasa ya kupakua makontena. Vilevile maboresho hayo yanahusisha bandari zilizopo katika maziwa zikiwemo Bandari za Kabwe, Katanga, Kibirizi pale Ujiji na Karema kule Mkoani Katavi katika Ziwa Tanganyika na Bandari ya Ndumbi katika Ziwa Nyasa na sasa tunakusudia kuimarisha Bandari ya Mbamba Bay katika Ziwa Nyasa hilo hilo ambako ujenzi wake utaanza siku za karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali bado kuna changamoto ya ufanisi mdogo wa bandari. Kutokana na hilo, Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya maboresho ya bandari ili kuongeza ufanisi lengo likiwa ni kuzifanya bandari zetu kufanya kazi kwa kiushindani wa kimataifa. Ili kufikia malengo hayo tunahitaji mifumo ya kisasa ya TEHAMA, maeneo ya kutosha ya

ndani na nje ya bandari kwa ajili ya maegesho ya meli na kuhifadhia shehena, pia na mitambo ya kutosha na ya kisasa ya kuhudumia shehena ambayo inagharama kubwa ya uwekezaji na uendeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tufikie malengo tuliyojiwekea tutapunguza msongamano wa meli baharini nje ya bandari, kupunguza muda mwingi unaotumika kupakua au kutoa mizigo bandarini ambao huleta athari mbalimbali zikiwemo kuongezeka kwa gharama za bidhaa kwa walaji na baadhi ya wafanyabiashara kutoka nchi jirani kukwepa kutumia bandari zetu na hivyo kusababisha Serikali kupoteza mapato ambayo yangetumika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kuwa Bandari ya Dar es Salaam ndiyo kitovu cha huduma za bandari hapa nchini. Ili kuiwezesha bandari hiyo kufanya kazi kwa ufanisi, kuongeza mapato ya nchi, ajira na kuchagiza sekta nyingine za kiuchumi Serikali iliamua kutafuta kampuni yenye uwezo na uzoefu mkubwa katika uendeshaji wa bandari duniani kwa teknolojia za kisasa.

Mheshimiwa Spika, suala hili lilileta msukumo kwa Serikali ya Tanzania na Serikali ya Dubai kuingia makubaliano kwa lengo la kuanzisha ushirikiano wa kiuchumi na wa kijamii katika uendeshaji wa maeneo ya bandari nchini ili kuwezesha kuipata Kampuni ya *DP World*. Kampuni hii imeonesha kuwa na utaalamu, teknolojia, uwezo na uzoefu mkubwa katika uendeshaji wa bandari 190 katika nchi 68 Barani Afrika, Asia, Ulaya, Amerika Kaskazini na Amerika Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa tarehe 10 Juni, 2023 Bunge lako tukufu lilipata fursa ya kuchangia, kuishauri Serikali na kupitisha Azimio la mapendekezo ya kuridhia makubaliano baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Dubai kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa bandari nchini. Nitumie nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yenu na ya

kuona umuhimu wa tija katika jambo hili na kuamua kupitisha Azimio lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na makubaliano hayo kumekuwa na maoni mbalimbali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, wanazuoni na wananchi kwenye baadhi ya vipengele vya makubaliano ambavyo tunapewa kuvizingatia wakati wa kufunga mkataba. Vipengele hivyo ni vile vinavyohusisha umiliki wa bandari, muda wa mkataba, ajira za wazawa, ulinzi na usalama wa nchi na manufaa yatakayotokana na mikataba itakayoingiwa na kwa upande mwingine baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na wananchi wameiomba Serikali kuwa makini mno ili mikataba itakayoingiwa katika uendeshaji wa maeneo ya bandari ya kukadiriwa iwe na tija kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makubaliano yaliyoingiwa sasa yanalenga kuweka msingi wa ushirikiano baina ya Serikali yetu ya Tanzania na Serikali ya Dubai. Maeneo ya uwekezaji yatakayopendekezwa ndiyo yatakayoingia mikataba kwa kila eneo na hivyo masuala ya mfumo wa uwekezaji kwa kutumia sheria za nchi yatazingatiwa. Mgawanyo wa mapato utazingatiwa, muda wa uwekezaji utajitokeza na ukomo wa uwekezaji huo utajadiliwa na kina na timu za majadiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu umiliki wa bandari nilihakikishie Bunge lako tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba kupitia Sheria ya Bandari ya mwaka 2004 Mamlaka ya Bandari Tanzania ndio iliyopewa mamlaka na haki ya kumiliki wa maeneo yote ya bandari nchini. Hakuna chombo chochote wala Mamlaka ya Bandari ambayo ina uwezo wa kutoa umiliki huo kwa kampuni yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wote wa utekelezaji wa makubaliano hayo na mikataba itakayoingiwa, vyombo vya ulinzi na usalama vitaendelea kutekeleza majukumu yao katika maeneo ya mradi kama ilivyofanya katika kipindi cha miaka yote 22 ya

mkataba na mwekezaji wa awali *TICTS* aliyemaliza mkataba wake mwezi Novemba, 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapato ninapenda kuwahakikishia Watanzania kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania itaendelea kusimamia masuala ya mapato Serikalini kutoka kwa mwekezaji kwa mujibu wa sheria na taratibu za mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya ufafanuzi nilioutoa kwenye masuala mbalimbali niliyoyaainisha Serikali yetu sikivu inawahakikishia Watanzania maoni na ushauri mliotupa Waheshimiwa Wabunge, wananchi na wadau ambao mmeshiriki kutoa maoni yenu mbalimbali, nataka niwahakikishie tutayazingatia. Aidha, Serikali itahakikisha kuwa mikataba ya utekelezaji itakayoingiwa itazingatia maslahi ya nchi na kuleta manufaa kwa Taifa letu. Kwa msingi huo nielekeze Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iendelee kuratibu utoaji wa elimu na ufafanuzi wa hoja za wananchi kuhusu na mikataba ili utofauti wa hatua hizi mbili uweze kuwa wazi kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwasihi Waheshimiwa Wabunge na wananchi tuendelee kuiunga mkono Serikali na kutambua dhamira yetu ya dhati ya kuwaletea maendeleo Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie pia nafasi kutoa rai kwa Watanzania wenzangu tusiruhusu mgawanyiko wa aina yoyote ile tunapotoa maoni yetu kuhusu uwekezaji wa aina yoyote ile nchini. Tuepuke kujadili kiitikadi za kisiasa, udini, ukabila, ukanda au vyovyote vile. Muhimu tuenzi tunu yetu ya amani na mshikamano wa Taifa letu uliodumu kwa miaka mingi na uliojengwa na waasisi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie ujenzi wa bandari ya uvuvi; sambamba na maboresho katika Bandari ya Dar es Salaam, Serikali inaendelea na ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Kilwa Masoko ambapo hadi sasa hatua zilizofikiwa ni kukamilika kwa

ujenzi wa ofisi za watumishi wa mkandarasi na mhandisi mshauri pamoja na eneo la hifadhi ya mafuta. Vilevile kuendeleza ujenzi na kazi ya kusimika mitambo katika eneo la kuzalishia zege, kukamilisha ujenzi wa eneo la kukatia vyuma na eneo la kuundia miundombinu ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa bandari hii ya uvuvi kutazalisha ajira, kutaongeza thamani ya mazao ya uvuvi kupitia miundombinu ya uhifadhi, uchakataji, masoko na hivyo kupunguza upotevu wa mazao. Vilevile kutaongeza tija kwenye shughuli za uvuvi wa kibiashara, uvuvi wa kati na uvuvi mdogo na kuwezesha meli kubwa za kibiashara zinazovua bahari kuu pamoja na meli za kimataifa, kutia nanga na kusafirisha samaki nje ya nchi wakitokea hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze utaratibu mpya wa utoaji mikopo na urejeshaji wa fedha zitokanazo na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri. Itakumbukwa kuwa, wakati tukiendelea na Bunge hili la bajeti, Serikali ilisitisha kwa muda utoaji wa mikopo inayotokana na asilimia 10 za mapato ya ndani ya Halmashauri ili kuweka utaratibu mpya ambao utawezesha Serikali kupata marejesho ya mikopo hiyo kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha hilo, Serikali iliunda kikosi kazi cha wataalamu ili kifanye kazi ya kuandaa mapendekezo ya utaratibu mpya wa utoaji wa mikopo na urejeshaji wa fedha hizo za mikopo. Kikosi kazi hicho kinaendelea kukamilisha taarifa yake ambayo itawezesha Serikali kufanya maamuzi na kuendelea kutoa mikopo kwa makundi mbalimbali. Taarifa ikishakamilika itawasilishwa ili Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote wapate uelewa kuhusu utaratibu mpya unaoelekezwa na Serikali. Nisisitize kuwa lengo la Serikali kutumia utaratibu mpya wa kutoa mikopo ni kuongeza ufanisi katika utoaji wa mikopo na urejeshaji wake ili iendelee kuhudumia walengwa wengine badala ya kuifanya mikopo hiyo itolewe kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kufuatia maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akihitimisha kilele cha Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani, namuelekeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI azingatie kuongeza kundi la waraibu katika wanufaika wa mikopo hiyo. Kila mkoa uweke mkakati wa haraka wa kuwaratibu waraibu wa dawa za kulevya, kuandaa kanzidata ili kundi hilo muhimu kwa nguvukazi yetu ili nalo pia liweze kunufaika na aina hiyo ya mikopo kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa na hivyo liweze kufanya shughuli za kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia Mkakati wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia; itakumbukwa kuwa tarehe 1 Novemba, 2022 Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa maagizo mahsusi yaliyolenga kumtua mama kuni kichwani. Dhamira hiyo ya Mheshimiwa Rais imetokana na athari ambazo jamii hususan kina mama wanakumbana nazo katika matumizi ya nishati zisizo safi za kupikia.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Rais aliagiza iandaliwe dira na mkakati utakaotoa mwongozo wa kitaifa wa kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia. Uamuzi huo ulilenga asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati hiyo ndani ya kipindi cha miaka 10.

Mheshimiwa Spika, maelekezo hayo ya Mheshimiwa Rais yalitaka ufanyike uchambuzi wa sera, sheria na miongozo iliyopo na kuanzisha mfuko maalum kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya nishati safi ya kupikia. Kadhalika kukataza matumizi ya kuni na mkaa kwa kupikia katika taasisi zinazoandaa chakula na kulisha watu zaidi ya 100 kwa siku. Taasisi hizo ni pamoja na shule, vyuo, magereza, viwanda na kambi za kijeshi.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha maono hayo ya Mheshimiwa Rais yanafanikiwa, Serikali imejipanga vyema kuendelea kusimamia

suala la nishati safi ya kupikia kwa kuweka mikakati madhubuti ikiwemo ifuatayo: -

Moja; kuongeza uelewa wa wananchi na taasisi kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia;

Mbili; kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa nishati safi, nafuu, endelevu na ya uhakika ya kupikia kupitia miundombinu ya gesi;

Tatu; kuandaa, kuoanisha na kuhuisha sera, sheria, kanuni na miongozo wezeshi itakayofanikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia;

Nne; kuhamasisha uwekezaji katika sekta ndogo ya nishati safi ya kupikia; tano; ni kuongeza wigo wa tafiti na ubunifu wa teknolojia zinazohusu nishati ya kupikia na sita; kujenga uwezo wa watekelezaji wa miradi ya nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuzielekeza Wizara, Idara na Taasisi za Umma kuandaa mpango kazi wa utekelezaji wa masuala ya nishati safi ya kupikia utakaowiana na dira yetu ili utekelezaji wake ukamilike ndani ya muda uliopangwa. Vilevile kila Halmashauri itengeneze mpango kazi kwa kuzingatia mazingira yake mahsusi na mchakato huu shirikishi kuanzia kwa wananchi hadi kwenye Mabaraza ya Madiwani.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwa tunapoondoka hapa Bungeni tukawe mabalozi wazuri wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia. Kitendo hicho kitasaidia kulinda mazingira na afya za Watanzania na kuimarisha nguvu kazi kwa ajili ya uzalishaji na maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mikakati ya udhibiti wa mmonyoko wa maadili; Serikali katika kulinda maadili na utu wa Mtanzania imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kudhibiti uhamasishaji

na kuenea kwa vitendo ambavyo ni kinyume na mila na desturi zetu kwa kuwa vinadhalilisha utu wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilielekeza Tume ya Kurekebisha Sheria kuzifanyia mapitio sheria zetu ili kubaini maeneo yenye udhaifu katika sheria zetu ambayo yanachangia au yanatoa mwanya wa kuenea kwa vitendo hivyo. Tayari Tume imeshafanya mapitio hayo ikiwa ni pamoja na kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali. Taarifa ikishakamilika itawasilishwa kwa hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imebuni mbinu za kitaifa za kukabiliana na changamoto hiyo kwa kushirikisha wadau wote muhimu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kazi hii inafanywa kwa ushirikiano mkubwa na wadau mbalimbali katika udhibiti wa mmomonyoko wa maadili.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine Serikali imeelekeza shule zetu zote kuendelea kutoa elimu kwa wanafunzi kuanzia ngazi ya elimu ya awali hadi kidato cha sita kuhusu madhara ya kujihusisha na vitendo hivyo. Suala hilo liende sambamba na kuimarisha madawati ya jinsia ili yaweze kutoa huduma kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo, Serikali imeendelea kuhimiza ushiriki wa jamii katika kukemea ukiukwaji wa maadili. Niwasihi sana Watanzania wenzangu tushirikiane kupaza sauti zetu ili tuweze kwa pamoja kukomesha vitendo hivyo ambavyo vinaweza kuleta athari kubwa kwa kizazi chetu cha sasa na baadaye. Serikali kwa upande wake itaendelea kuwachukulia hatua kali wale wote watakaothibitika kuhamasisha na kujihusisha na vitendo vya ukiukwaji wa maadili. Nirudie kusisitiza suala hili sio la Serikali peke yake, tunahitaji ushirikiano wa kila Mtanzania katika kukomesha vitendo hivyo ambavyo vinatishia ustawi wa nguvu kazi hapa nchini. Hatuna budi sasa kulinda vizazi vyetu dhidi ya tamaduni za kigeni zinazohatarisha ustawi na maendeleo ya Taifa ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelekezo mahsusi kwenye maeneo yafuatayo; sote tunatambua kuwa hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimekuwa chachu ya maendeleo katika sekta mbalimbali hapa nchini. Katika kuunga mkono jitihada hizo za Mheshimiwa Rais, nami pia ningependa kusisitiza na kuelekeza masuala muhimu yafuatayo:-

Moja; Taasisi za Serikali kukamilisha malipo ya huduma na malimbikizo ya tozo na michango ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya waajiri kutotunza kumbukumbu za michango ya waajiriwa, kutowasilisha kwa wakati malimbikizo ya michango na tozo za watumishi katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hali hiyo imekuwa ikisababisha usumbufu kwa watumishi pindi wanapostaafu. Ninaelekeza waajiri watunze kumbukumbu za malipo ya michango ya waajiriwa pamoja na kulipa malimbikizo ya michango ya watumishi na tozo katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ifikapo tarehe 30 Septemba, 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya taasisi zimekuwa zikichelewesha malipo au kutolipia kabisa huduma wanazozipata kutoka taasisi nyingine za Serikali ikiwemo huduma za maji, umeme, simu, pango na ujenzi na hivyo kuathiri utendaji wa taasisi husika. Ninazielekeza taasisi zote za Serikali kulipia huduma hizo wanazopata kutoka taasisi nyingine ikiwemo Shirika la Umeme *(TANESCO),* Shirika la Mawasiliano *(TTCL),* Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC),* Wakala wa Majengo *(TBA)* na Mamlaka za Maji ifikapo tarehe 30 Septemba, 2023 ili kuepusha kukwamisha utendaji wa taasisi zetu.

Mbili; kusimamia uhifadhi wa mazao ya chakula; Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya kuhifadhia chakula kwa ajili ya kuimarisha hali ya usalama na upatikanaji wa chakula nchini. Licha ya hayo, imetoa kipaumbele cha ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mazao ya nafaka na vyumba vya baridi vya kuhifadhia

mazao yanayoharibika ndani ya muda mfupi kama mboga mboga na matunda.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usalama wa chakula, Serikali imetenga shilingi bilioni 320 kwa ajili ya ununuzi wa nafaka kupitia Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula *(NFRA)*. Hivyo basi, ninamuelekeza Waziri wa Kilimo kusimamia zoezi la ununuzi wa nafaka ili liweze kufanyika kwa wakati na kwa ufanisi. Vilevile nitumie nafasi hii kuwakumbusha wananchi umuhimu wa kuhifadhi chakula katika ngazi ya kaya na kuepuka matumizi ya chakula yasiyo sahihi.

Tatu; ni kuboresha mifugo na kutatua migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi; sekta ya mifugo ina umuhimu mkubwa kutokana na mchango wake katika ajira, mapato na lishe inayotokana na mazao yake ikiwemo nyama na maziwa. Hata hivyo, mchango wa sekta ya mifugo hapa nchini ni mdogo ikilinganishwa na idadi ya mifugo iliyopo kutokana na ufugaji usio na tija. Ufugaji huo umesababisha wafugaji na Taifa kwa ujumla kuendelea kupata mapato kidogo. Kwa upande mwingine ufugaji wa aina hiyo umekuwa ukichochea migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ikiwemo wakulima.

Mheshimiwa Spika, kila jambo lina wakati wake, ni imani yangu kuwa wakati umefika wa kuwa na mifugo bora na yenye tija ambayo itaongeza kipato cha wafugaji wetu sambamba na kutatua migogoro inayotokana na ufugaji usio na tija. Kwa msingi huo, ninaelekeza masuala yafuatayo kwenye eneo hili la mifugo.

Moja, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iweke msukumo wa kutosha katika uboreshaji wa mifugo hapa nchini ili wafugaji waache kuchunga na badala yake wafuge ili wawe na mifugo bora na yenye tija. *(Makofi)*

Mbili, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iimarishe uratibu wa mifugo na kuwaelimisha wafugaji kufuga kwa tija na kuwa na idadi ya mifugo inayolingana na uwezo wa maeneo waliyonayo. Hatua hii

iende sambamba na kumiliki maeneo na kupanda nyasi kwa ajili ya malisho.

Tatu, Mamlaka za Vijiji zibainishe wafugaji waliopo kwenye maeneo yao na kutenga maeneo rasmi kwa ajili ya ufugaji wao sambamba na kutopokea wafugaji wapya endapo hakuna eneo la malisho linalotosha kwa wafugaji wanaohamia ili kuepusha migogoro. Vilevile nitoe rai kwa wafugaji wafuate taratibu za kuhamia kwenye vijiji endapo kutakuwa na ulazima wa kuhama kutoka kijiji kimoja kwenda kingine.

Nne, elimu kuhusu ufugaji bora na wenye tija unaofanyika kwa baadhi ya maeneo hapa nchini isambazwe ili inufaishe wafugaji wa maeneo mengi zaidi na hivyo kuongeza tija kwa wafugaji; na tano, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ishirikiane na Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kubainisha na kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za ufugaji wakati wa utekelezaji wa miradi ya upangaji wa miji na vijiji ikiwemo Mradi wa Kuboresha Usalama wa Milki Ardhi Nchini *(LTIP)*.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne, uhifadhi wa mazingira na upatikanaji wa maji; kwa kutambua umuhimu wa suala la uhifadhi wa mazingira, tarehe 27 Aprili, 2023 nilitumia kipindi cha maswali ya papo kwa papo cha Bunge lako kuelezea hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kulinda, kutunza na kufanya maliasili zetu kuwa endelevu kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo. Maliasili hizo ni pamoja na hifadhi za wanyamapori, hifadhi za misitu, mito na vyanzo vya maji ambavyo uendelevu wake unategemea ushiriki wetu katika kuvitunza, kuvihifadhi na kuvilinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa maji kwa wananchi, ninasisitiza na kuelekeza masuala yafuatayo:-

(i) Wizara ya Maji idhibiti upotevu wa maji wakati wa kusambaza maji kwa wananchi sambamba na kufufua visima vya zamani ambavyo vina maji kwa wingi na havitumiki ili kuwezesha maji

kupatikana kwa wingi kwenye maeneo yote na katika vipindi vyote vya mwaka.

(ii) Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lifanye tathmini ya uharibifu wa mazingira nchini na kuweka mikakati itakayowezesha shughuli za kilimo, umwagiliaji na ufugaji kufanyika bila kuharibu vyanzo vya maji na maeneo yaliyohifadhiwa.

(iii) Mamlaka za Mabonde zisimamie kikamilifu vibali vya matumizi ya maji kwa kuzingatia mahitaji ya watumiaji wengine na uendelevu wa upatikanaji wa maji katika maeneo husika, pamoja na kuendelea kuelimisha wananchi kuhifadhi vyanzo vya maji na maeneo yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, eneo la tano, upangaji wa miji na utatuzi wa migogoro ya umiliki wa viwanja; mahitaji ya uendelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwemo kuanzisha makazi yameendelea kuongezeka. Ongezeko hilo ni muhimu likazingatiwa katika upangaji wa miji yetu hapa nchini. Kwa msingi huo, nizielekeze Halmashauri zote kupima maeneo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwemo viwanja kwa ajili ya makazi badala ya kuacha wananchi kujenga kiholela sambamba na kuweka utaratibu mzuri wa ugawaji wa viwanja ili kuepuka kiwanja kugawiwa kwa mmiliki zaidi ya mmoja na kusababisha migogoro isiyokuwa muhimu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi kwenye maeneo mbalimbali nchini ikiwemo hapa Jijini Dodoma ya kutolipwa fidia baada ya maeneo yao kutwaliwa na Halmashauri ya Jiji. Nitumie fursa hii kuzielekeza Halmashauri zote nchini kuhakikisha maeneo yanayotwaliwa kutoka kwa wananchi yanalipiwa fidia kwa wakati ili kuepusha migogoro inayoweza kujitokeza siku za usoni.

Sita, kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya mwaka 2023/2024; katika Mkutano huu Bunge lako tukufu limepitisha Mpango wa Bajeti ya mwaka 2023/2024 ambao unaakisi dhamira

njema ya Rais wetu ya kuwaletea maendeleo wananchi. Utekelezaji wa mpango huo utawezesha kufanyika kwa shughuli za kiuchumi na kijamii zinazogusa maisha ya wananchi wetu, hivyo nitumie fursa hii kuelekeza masuala yafuatayo: -

(i) Maafisa Masuuli waimarishe usimamizi wa matumizi ya fedha za umma na kutekeleza kikamilifu mpango wa bajeti wa 2023/2024.

(ii) Wizara na Taasisi za Serikali zifanye vikao kwa njia ya mtandao kila inapowezekana na bila kuathiri tija ili kupunguza matumizi makubwa ya fedha za umma na gharama zisizo za lazima na uendeshaji wa vikao vya Serikali.

(iii) Watendaji wa Serikali wazingatie kanuni, sheria na taratibu katika manunuzi na matumizi ya fedha za umma ili kufikia shabaha na malengo ya uchumi

(iv) Watendaji wa Serikali waimarishe ukusanyaji wa mapato na kufanya matumizi kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2023/2024 sambamba na kubuni vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Spika, nikiwa namalizia naomba nihitimishe kwa eneo la michezo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa jitihada na hamasa zake ambazo zimegeuzwa taswira nzima ya Tanzania katika medali za michezo kikanda na kimataifa. Tumeshuhudia akitoa motisha katika mashindano mbalimbali na kuongeza hamasa, mashindano na hatimaye bendera yetu imezidi kupepea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais na kufanya jitihada za kuinua michezo mbalimbali hapa nchini kuwa ni

jitihada zenye malengo ya mafanikio. Nitumie fursa hii pia kuwapongeza wanamichezo wetu nchini ambao wametutoa kimasomaso katika mashindano mbalimbali ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza mwanariadha wetu Gabriel Geay kwa kushika nafasi ya pili katika mashindano makubwa na maarufu Duniani ya *Boston Marathon* pamoja na yale ya *Valencia Marathon. (Makofi)*

Pili nimpongeze sana Alphonce Felix Simbu aliyeshika nafasi ya tatu katika Mashindano Maarufu Duniani ya *Osaka Marathon* pamoja na yale ya *Guangzhou Shenzhen Half Marathon* nyote mnakubaliana nami kuwa tunayo hazina ya vipaji vya wanariadha si tu hao wawili wako wengine ambao pia wanafanya vizuri kwenye riadha hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili nitoe msisitizo kwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuibua wanariadha zaidi na kuwafuatilia kwa karibu maendeleo yao, kuwatangaza na kuwakutanisha na fursa muhimu zilizopo, kuwatafutia mashindano mbalimbali ya ndani na nje ya nchi ili wajiendeleze zaidi kwa viwango vya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mchezo wa ngumi al–maarufu masumbwi, nampongeza sana mwanamasumbwi Twaha Kiduku ambaye tarehe 22 Aprili, 2023 huko Morogoro alimtwanga Iago Kiziria wa Georgia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia mwanamasumbwi Hassan Mwakinyo ambaye tarehe 23 Aprili, 2023 alimtwanga Kuvesa Katembo wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunao pia wapiganaji wetu maarufu ambao wanajiandaa kwenye mashindano yanayofanya vizuri akiwemo mpiganaji Mfaume Mfaume, Ibrah Class, Dulla Mbabe, Kidunda na Mandonga. Hawa wanaendelea kufanya vizuri zaidi,

wanaendelea kulipaisha Taifa letu kwenye mchezo huo wa masumbwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tunao kwa upande wa ngumi za wanawake; nampongeza sana mwanadada shupavu Fatuma Yazidu ambaye tarehe 23 Machi, 2023 alimshinda kwa alama nyingi Consolata Musanga kutoka Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunaona namna wanawake wanavyojitokeza kucheza mchezo huu wa ndondi wakiwemo Stumai Muki, Zulfa Macho, Nasra, Mariana Msabila na wengineo. Katika eneo hili bila kumsahau mdhamini wa michezo ya ndondi kwa wanawake Mheshimiwa Mwakagenda (Mb), hakika Mheshimiwa Mwakagenda ametupa heshima Bunge letu kwa kuwa mdhamini wa ndondi ya wanawake Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudie tena eeh?

**WABUNGE FULANI:** Eeh.

**WAZIRI MKUU:** Hakika Mheshimiwa Mwakagenda, Mbunge ametupa heshima Waheshimiwa Wabunge na Bunge letu tukufu kwa kuwa mdhamini wa mashindano haya ya ndondi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo sitaishukuru sana Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa na wadau wengine kwa jitihada zao zinazowezesha kurejesha umaarufu wa mchezo wa ngumi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile navipongeza sana vyombo vya habari hususan *tv* kupitia kipindi cha vitasa kwa kuwa vinara katika kuonyesha, kutangaza na hivyo kuleta msisimko katika mchezo huo wa ngumu ambao sasa unachukua nafasi kubwa Barani Afrika katika siku za hivi karibuni ulikuwa umeanza kupoteza umaarufu wake hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mchezo wa mpira wa miguu; nitumie fursa hii kuipongeza Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania kwa jitihada na mikakati ya makusudi ya kuendeleza mchezo wa soka hapa nchini. Nyota njema huonekana asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia timu yetu ya Taifa au *Taifa Stars* ikianza vyema hivi karibuni katika michezo ya kufuzu Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika *(AFCON)*. *Taifa Stars* ilifanikiwa kutoka kidedea kwa ushindi wa goli moja dhidi ya timu ya Niger. Naipongeza sana *Taifa Stars* kwa ushindi huo, niungane na Watanzania wenzangu kuunga mkono timu yetu ya Taifa na kuitakia kila la kheri katika michezo iliyobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nivipongeze sana vilabu vyote vilivyoshiriki katika ligi mbalimbali hapa nchini. Hakika mmekuwa mkikonga mioyo ya Watanzania kwa kucheza mpira wa viwango vya juu na kuifanya Ligi Kuu ya Tanzania kuwa ligi kuu bora ya tano Afrika, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie basi fursa hii kuvipongeza vilabu vyetu vya Simba na Yanga kwa kutuwakilisha vyema katika Mashindano ya Vilabu Barani Afrika. *(Makofi)*

Nianze kwa kuipongeza Timu ya Simba kwa kushiriki michuano ya Klabu Bingwa Barani Afrika na kuchuana na miamba ya soka Bara la Afrika, nawapongeza sana kwa kufanikiwa kufikia hatua ya robo fainali ambapo inapambana na timu ya Wydad Casablanca ya Morocco, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niipongeze timu ya *Dar Young African* al–maarufu mwananchi. Haya inatosha… *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hawana tawi hata Bungeni hapa. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nirudie vizuri, isikike vizuri. Niipongeze sana timu ya *Dar Young African*, timu ya wananchi

kwa heshima kubwa waliyoiletea Taifa letu kwa kufanikiwa kwa mara ya kwanza kucheza fainali katika Mashindano ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika fainali hiyo Yanga ilifanikiwa kuigaragaza nyumbani kwao timu ya USM Alger kutoka nchini Algeria kwa bao moja kwa nunge na sote tunatambua timu ya Yanga haikutwaa ubingwa kutokana na timu ya USM Alger kupata magoli mawili ya ugegeni. Kitendo kilichopelekea Yanga kushika nafasi ya pili na kutunikiwa medali ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami niungane na Watanzania kuwapongeza Wanayanga kwa hatua hiyo muhimu na mshikamano mliouonesha wakati wote wa mashindano kufikia hatua hiyo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili nirudie kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alikuwa bega kwa bega na vilabu vyetu kwa kuvipa motisha ili viweze kusonga mbele ikiwemo na kuwaalika wacheza wa vilabu vyetu ikiwemo na Yanga pale kwenye jengo letu maarufu nchini, Ikulu kwa ajili ya kupata neno na nasaha muhimu ya michezo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa msimu huu umekuwa bora sana kwa timu zetu za ligi kuu kwa mafanikio hayo niliyoyaeleza awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza tena Wizara, Shirikisho la Soka Tanzania, vilabu na uongozi wote, wadhamini na wachezaji wote, kwa sasa tunalo jukumu la kujenga uwezo wa wachezaji wetu wa ndani ili kupanua na kunufaika na soko la ajira katika michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu, nitumie fursa hii kuwashukuru sana watendaji wote wa Serikali kwa jitihada na ushauri wa kitalamu ambao umewezesha kwa kiasi

kikubwa mafanikio ya shughuli zilizopangwa kwenye mkutano huu kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia namshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuishauri vyema Serikali katika kipindi chote cha Bunge. Namshukuru pia Katibu wa Bunge na watumishi wote wa Bunge kwa huduma nzuri mliyotupatia wakati wa kipindi chote cha Bunge hapa kwenye Bunge hili la Bajeti, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nivishukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi yenu nzuri. Tumeishi kwa amani na utulivu katika kipindi chote cha Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi na Mbili. Nawashukuru sana wanahabari kwa kazi kubwa mliyoifanya ya kuwafikishia taarifa mbalimbali Watanzania na kote duniani na kuhakikisha kwamba wananchi wanapata habari za mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukurani nyingi ziwaendee madereva wetu waliotuhudumia wakati wote tukiwa safarini kuja hapa na huduma za kila siku hapa Jijini Dodoma na maeneo ya jirani. *(Makofi)*

Lakini pia nitoe shukrani kwa watoa huduma wengine walioshiriki kutuhudumia muda wote tukiwa hapa Dodoma tunatambua tunao watoa huduma nje ya geti pale jirani wao wamesaidia sana kufanya utulivu kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nakushukuru wewe nafasi yako ni kubwa sana. Tuendelee kukushukuru sana kwa kazi nzuri uliyoifanya katika kipindi hiki na hii ndiyo ambayo imepelekea Bunge hili kupata mafanikio na kupita karibu mpango wote wa Serikali ambao tumeuleta kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii pia kuwatakia kila la kheri Waheshimiwa Wabunge pamoja na shukrani za ushirikiano mzuri mlioutoa kwa Serikali wakati wote tulipokuwa tunaleta jambo

letu kwenye Bunge letu mmeweza kuunga mkono, lakini mmeweza pia kutoa ushauri, mmeweza kutoa maoni. *(Makofi)*

Nirudie tena kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba tutaendelea kutekeleza yale yote mliyotushauri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wenzangu niwatakie safari njema na mnaporejea majimboni kwenu. Niwaombe mkaendelee kutoa ufafanuzi kuhusu mambo muhimu yaliyojitokeza katika kipindi hiki chote cha Bunge, wajulisheni wananchi kuhusu vipaumbele vilivyopo kwenye bajeti ya mwaka 2023/2024 na kuwasihi waendelee kuinga mkono katika kusimamia utekelezaji wake. Nendeni mkawahakikishie dhamira ya Serikali njema ya kuwaletea maendeleo pamoja na dhamira ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuleta maendeleo kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatarajia kwamba kesho tarehe 29 Juni, 2023 kutakuwa na Sikukuu ya Eid el Hajj. Nitumie fursa hii kuwatakia waislamu wote na Watanzania wote kwa ujumla maadhimisho mema na yenye baraka katika sikukuu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninapenda kutoa hoja kuwa Bunge lako tukufu liahirishwe hadi tarehe 29 Agosti, 2023 siku ya Jumanne saa 3.00 asubuhi tutakapokutana tena katika Ukumbi huu hapa Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji; Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuliairisha Bunge mpaka tarehe aliyoitaja. *(Kicheko/Makofi)*

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

**SPIKA:** Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya Afrika Mashariki.

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliimbwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa hoja ambayo umeileta hapa Bungeni ya kuairisha Bunge na hoja na hiyo imekubaliwa na Bunge kwa kura nyingi. Kwa hiyo, tunakushukuru sana kwa hotuba ambayo umeeleza mambo kwa kifupi yale ambayo Bunge limefanikiwa kuyafanya katika kipindi hiki, lakini pia umetueleza kwa ufupi kwa upande wa Serikali ambayo imefanikiwa kuyafanya katika kipindi hiki.

Tunakushukuru sana kwa ushirikiano ambao umeutoa hasa katika kipindi kile ambacho huwa unaulizwa maswali ya moja kwa moja lakini pia kwa usimamizi wa jumla wa Serikali hapa Bungeni tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pia nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote wakiongozwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayesimamaia Sera, Bunge na Uratibu, ameonesha ushirikiano mkubwa sana kuanzia kwenye ngazi ya Kamati walipokuwa wanaleta Makadirio ya Mapato na Matumizi,

wamekuja na Maafisa Masuuli wao tunawashukuru sana kwa ushirikiano. *(Makofi)*

Lakini pia nitumie fursa hii nikiwashukuru ninyi nimewashukuru pia Naibu Mawaziri ahsanteni sana kwa kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge vizuri sana tunawapongeza nanyi pia. *(Makofi)*

Kwa kusema hayo niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote mmefanya kazi kubwa sana na kwa uzalendo kwa kweli wa hali ya juu, kipindi hiki kilikuwa ni kirefu, lakini wote mmekuwa na utulivu na mmefanya kazi kuanzia ngazi ya Kamati na baadaye hapa Bungeni mmetoa mawazo yenu mengi ambayo Serikali imeyachukua, imeyafanyia kazi mengine tukiwa hapa hapa na ndio maana kulikuwa na marekebisho ya hapa na pale kwenye Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na mengine wameahdidi Mawaziri hapa wakati wakihitimisha hoja zao kwamba michango yenu mliyoitoa itaenda kuisaidia Serikali katika kuboresha utendaji kazi wake. Kwa hiyo, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia niwashukuru sana Wenyeviti wa Kamati na Makamu Wenyeviti kwa kazi nzuri waliyoifanya nadhani sote ni mashahidi kwamba wamesimamia Kamati zao vizuri na kwa kuzisimamia Kamati zao vizuri tumeweza kufanya vizuri sisi sote kama Bunge. *(Makofi)*

Pia niwashukuru sana Wenyeviti sasa wa Bunge ambao wananisaidia kazi hapa. Ninawashukuru sana, sana kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya kwa kipindi chote cha usimamizi wa hoja hapa Bungeni. Ahsante sana Mheshimiwa Najma Murtaza Giga ahsante sana, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile nakushukuru sana na nakushukuru sana Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kipekee kabisa nimshukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa usaidizi wake ambao na yeye

amefanya kazi kubwa sana ya kunisaidia katika kusimamia vikao hapa lakini na mambo mengine kuniwakilisha huku na huko, ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa usaidizi ambao umenipa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nimshukuru Katibu wa Bunge kwa uratibu mzuri yeye na maafisa wake wote, mmefanya kazi kubwa, kazi nzuri kwa kweli tunawashukuru sana, sana na hata wale ambao wako maofisini muda huu, basi utawapelekea ujumbe huo tunawashukuru sana kwa kazi nzuri. Wale ambao ni Makatibu wa Kamati, lakini na wale ambao wanabaki ofisini kwa sababu ndio wanafanya uratibu wa hizi Kamati tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia niwashukuru sana pamoja na kuwashukuru wote mlioko humu ndani na ndio wawakilishi wa wananchi, lakini nitumie nafasi hii kuwashukuru pia wananchi wametoa mawazo yao katika maeneo mbalimbali, wengine wametoa kupitia ninyi kwa hivyo nimeshawashukuru, lakini wale ambao walileta mawazo yao moja kwa moja kupitia njia mbalimbali yote hayo tuliyapokea na mengine tumefanikiwa kuyafanyia kazi na yale ambayo hatukuyafanyia kazi basi wajue tumeyasikia na tutayafanyia kazi wakati utakapofika. Kwa hiyo nawashukuru wananchi wote kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na kwa kusema hayo nimalizie kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunamshukuru kwa ushirikiano wake anaoutoa kwanza yeye kama sehemu ya Bunge, lakini yeye pia kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anatupa ushirikiano mkubwa sana Bunge, lakini pia anafanya kazi nasi kwa karibu jambo ambalo linatusaidia hata sisi kufanya kazi yetu kwa ufanisi. Kwa hiyo, tunamshukuru sana kwa ushirikiano huo na tunampongeza pia kwa kusikiliza mawazo ya Waheshimiwa Wabunge na hapa ningeweza kutaja mambo mengi,

nilitaje moja tu Waheshimiwa Wabunge kwa kuturejeshea Tume ya Taifa ya Mipango, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka mlichangia jambo hili kwa nguvu sana kuanzia mwaka jana na tukaletewa hapa muswada tumepitisha katika Bunge hili, kwa hiyo, hiyo inaonesha namna ambavyo Waheshimiwa Wabunge mawazo yenu Serikali inayafanyia kazi na Serikali yetu ilkiongozwa na Mheshimiwa Rais na yeye tunamshukuru sana na kwa kweli pia kwa uvumilivu wake, mambo yako mengi, lakini bado ameendelea kuonesha msimamo yeye kama kiongozi wa nchi katika kuisimamia nchi, lakini pia kuisismia Serikali ili iweze kutekeleza majukumu yake. Tunamshukuru sana na kumpongeza sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hapo ningeweza sasa kuanza na salamu nyingine, lakini salamu zinazonihusu mimi pia nizipokee kutoka kwenu nyote ninawashukuru sana kwa salamu mlizozitoa zinazonihusu mimi na Mheshimiwa Waziri Mkuu nadhani amezitoa kwa ujumla, kwa niaba yetu sisi sote Wabunge, lakini pia kwa niaba ya Serikali, ninakushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimezipokea kwa unyenyekevu kabisa. *(Makofi)*

Waheshimwa Wabunge, wakati nikimalizia kulikuwa na mambo matatu ambayo yalijitokeza katika Bunge hili na kwa sababu tunamaliza leo, nitataka tuyamalize kwa sura hii.

Jambo la kwanza ni lile jambo ambalo lililojitokeza hapa lililokuwa linahusu kushika shilingi Mheshimiwa Godwin Kunambi, alileta barua ofisini na ameshajibiwa, kwa hiyo halikuulizwa hapa Bungeni, kwa hivyo watu wasije wakawa wanaona hapa mengine yamejibiwa na hilo halijajibiwa, kwa hivyo yeye amejibiwa kwa barua, lakini kwa ujumla wake jambo lile namna lilivyofanyika hapa Bungeni kwa mujibu wa kanuni zetu, maana kanuni ziko nyingi kwa hiyo hutegemea unataka kupita njia gani. Kwa njia yoyote ile ambayo sisi tumezipitia hizo kanuni suala lile lilivyofanyika hapa Bungeni lilikuwa sawasawa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine mambo mawili sasa maana nilisema matatu; jambo lingine mtakunbuka siku ya tarehe 27 Mheshimiwa Jenista Mhagama aliomba kuhusu utaratibu baada ya Mheshimiwa Mpina kutoa mchango wake, sasa kwa sababu hii miongozo miwili ni mirefu kidogo na kwa sababu tumetoka kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, miongozo hii itaingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, lakini nitoe maamuzi yale ya jumla. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa maamuzi ya jumla kama nilivyosema mtaenda kusoma kwenye Taarifa Rasmi za Bunge inaenda kuwekwa huko, lakini kwa ufupi Mheshimiwa Mpina alikuwa amechangia kuhusu makatazo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa ameyatoa hapa Bungeni na kwamba matukio haya yalikuwa yakindelea huko nje na yeye Mheshimiwa Jenista alipoomba Kuhusu Utaratibu Mheshimiwa Mpina kaleta vielelezo vyake ofisini kama alivyokuwa ametakiwa, lakini pia na mchango wake aliokuwa ameutoa hapa baada ya kupitia Taarifa Rasmi za Bunge ya mchango aliokuwa ameutoa na maelekezo aliyokuwa ameyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumejiridhisha kwamba wakati Mheshimiwa Mpina akichangia na ule mchango wake na maneno aliyokuwa ameyasema, alikuwa sahihi kwa sababu maelekezo yale yalikuwa hayajaanza kufanyiwa kazi bado. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mtayapitia hayo kwenye Taarifa Rasmi za Bunge lakini kwa ujumla hilo jambo linamalizwa kwa namna hiyo. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA KUHUSU USHAHIDI ULIOWASILISHWA NA MHE. LUHAGA JOELSON MPINA JUU YA KUPUUZWA KWA MAAGIZO YA WAZIRI MKUU KUHUSU KUENDELEA KWA OPERESHENI ZA KUKAMATA WAFUGAJI BAADA YA TANGAZO LAKE LA TAREHE 27 APRILI, 2023 - KAMA ULIVYOANDALIWA

**Waheshimiwa Wabunge,** mtakumbuka kuwa mnamo tarehe 3 Mei, 2023 Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) wakati akichangia mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo

na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 alilieleza Bunge kuwa hivi sasa operesheni za kamatakamata ya mifugo zimekithiri maeneo mbalimbali nchini ambapo Askari wa Wanyamapori na Watendaji wengine wa Serikali wanaendesha operesheni ya ukamataji mifugo kiholela na bila kuzingatia sheria kama vile Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya Mwaka 2013 *(The Animal Disease Act No. 17 of 2023),* Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya Mwaka 2008 na Kanuni ya *The Animal Welfare Impounded Animal Regulation 2020*.

**Waheshimiwa Wabunge,** katika kuhitimisha hoja yake hiyo Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) alieleza kuwa, nanukuu "***Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu alitoa tamko hapa la kuzuia hayo mambo kutokea, lakini mambo hayo yamekuwa yakiendelea, mimi siamini kama wale Watumishi wana uwezo wa kuzuia maelekezo ya Waziri Mkuu, isipokuwa Waziri Mkuu mwenyewe anaruhusu haya mambo yafanyike na yanafanyika kwa ridhaa yake."*** Mwisho wa kunukuu.

**Waheshimiwa Wabunge,** baada ya maelezo hayo ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) alisimama Mheshmiwa Jenista Joakim Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Wazri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) akiomba "Kuhusu Utaratibu", nami ikanilazimu kusimamisha mchango wa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) ili kumpa nafasi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Wazri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) afafanue kuhusu Kanuni ya Bunge iliyokuwa inavunjwa.

**Waheshimiwa Wabunge,** Mheshmiwa Jenista Joakim Mhagama alisimama chini Kanuni ya 75 ya Kanuni za Kudumu za Bunge "*Kuhusu Utaratibu*" ambapo alilieleza Bunge kuwa Kanuni inayovunjwa na Mchangiaji ni Kanuni ya 71(1)(a) ambayo inakataza Mbunge kutoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

**Waheshimiwa Wabunge,** Mheshmiwa Jenista Joakim Mhagama aliendelea kulieleza Bunge kwamba Mheshimiwa Mpina amemtuhumu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba ni chanzo cha kutotekelezwa kwa utendaji bora kwenye masuala ya kutetea Wafugaji na Kusimamia Haki za Wafugaji na kwamba Taarifa

zilizotolewa na Mheshimiwa Mpina hazina ukweli, kwa sababu ni juzi tu Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa kauli ndani ya Bunge kuonyesha ni kwa kiasi gani Serikali itashughulikia migogoro ya Hifadhi na kuhakikisha pia malalamiko ya Wabunge, malalamiko ya Watanzania na Maazimio ya Bunge yanafanyiwa kazi ipasavyo ili kulinda heshima ya Serikali na heshima ya Wabunge na vile vile kujali hali na malalamiko ya Watanzania katika maeneo yao.

**Waheshimiwa Wabunge,** mtakumbuka baada ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Wazri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) nilisimama na kufafanua kwamba, nanukuu "***mimi nimemsikiliza Mheshimiwa mpina, ameeleza maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu huko nyuma, na kwa kwamba hayo maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu hayafuatwi katika hili eneo analochangia yeye, na muktadha huo ndiyo, anasema, ikiwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelekezo na hayafuatwi na wale wanaopaswa kuyafuata, basi maana yake mtoa maelekezo, yeye mwenyewe pia anaona sawa.***"

**Waheshimiwa Wabunge,** katika kutaka ufafanuzi zaidi ili niweze kutoa mwongozo wangu juu ya suala hilo, nilimpa nafasi nyingine Mheshimiwa Waziri ili kujua kwamba katika maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo Mheshimiwa Mpina anayazungumzia, Je, ni kweli aliyoyasema ama hayapo? Kama yapo, Je, yamefanyiwa kazi au hapana? Na kama yapo maelekezo na hayajafanyiwa kazi, hoja ya Mheshimiwa Mpina ni kwamba ikiwa mtoa maelekezo (Waziri Mkuu) mwenyewe anaona mambo haya yanafanyika basi yanafanyika kwa ridhaa yake.

**Waheshimiwa Wabunge,** Mheshmiwa Jenista Joakim Mhagama kwa mara nyingine alisistiza na nanukuu ***"Mheshimiwa Spika, nadhani wote tumemsikia Mheshimiwa Mpina maelezo aliyoyatoa Bungeni. Maeneo yote ambayo Mheshimiwa Mpina anayazungumzia kwa muktadha wake yanahusu migogoro inayowahusu Wafugaji ambayo Mhe. Waziri Mkuu aliyajumuisha kwenye Taarifa yake akionyesha yaliyofanywa na Serikali na Maelekezo ya ziada kwa***

***Mawaziri na Serikali kuhakikisha mambo hayo yote yanafanyiwa kazi ipasavyo."*** Mwisho wa kunukuu.

**Waheshimiwa Wabunge,** baada ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) nililazimika kumuagiza Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) awasilishe ushahidi wa madai aliyoyatoa wakati wa mjadala kuhusu kupuuzwa kwa maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ifikapo tarehe 9 Mei, 2023 ili niweze kutoa mwongozo wangu juu ya jambo hilo.

**Waheshimiwa Wabunge,** mnamo tarehe 9 Mei, 2023 Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) alitii maagizo yangu kwa kuwasilisha vielelezo vya ushahidi juu ya jambo hilo kama nilivyomuagiza. Vielelezo hivyo ni kama ifuatavyo:-

1. **Kiambatisho Na. 1.** Barua ya Mheshimiwa Hussein Nassor Amar (Mb) Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale Mkoa wa Geita akielezea Wafugaji wake ambao tarehe 1.5.2023 baada ya agizo la Waziri Mkuu kutolewa tarehe 27 Aprili, 2023 ambapo jumla ya wafugaji 26 walikamatwa wao na mifugo yao jumla ya ng'ombe 541 ambapo walipigwa faini ya jumla ya sh. 25,600,000 wastani wa shilingi 47,319 kwa kila ng'ombe kinyume cha Sheria.

2. **Kiambatisho Na. 2.** Barua ya Mheshimiwa Fransis Mtega (Mb) Mbunge wa Jimbo la Mbarali ambapo tarehe 6 Mei, 2023 Helkopta ilishuka na Wafanyakazi wa TANAPA huko Mwanavala na wakaanza kuswaga ngo'mbe ziende eneo la hifadhi wananchi walipojaribu kuzuia walipigwa sana ambapo Ndugu Golyama Ihimya alipigwa na kujeruhiwa vibaya na kwenda kulazwa katika Hospitali ya Rujewa Mission huko Mbarali Mkoa wa Mbeya. PF3 na picha zimeambatishwa.

3. **Kiambatisho Na. 3** Barua ya tarehe 04 Mei, 2023 kuhusu Malalamiko ya wafugaji wa Kijiji cha Namwawala Wilaya ya Kilombero Mkoa wa Morogoro ambapo wafugaji 21 wenye jumla ya ng'ombe 2082 wamekamatwa na Polisi na watu wa TAWA kwa amri ya Mkuu wa Wilaya ya Kilombero. Mifugo hiyo

ilikuwa kijijini na ilifunguliwa kwenye mazizi ya wafugaji na kwenda kushikiliwa katika Gereza bila usimamizi mzuri na inaendelea kufa.

4. **Kiambatisho Na. 4.** Malalamiko ya Wafugaji wa Kaliua Mkoa wa Tabora ambapo tarehe 29 Aprili, 2023 mifugo yao ilikamatwa ikiwa kwenye mazizi majira ya usiku.

5. **Kiambatisho Na. 5.** Barua ya taarifa ya kukamatwa ng'ombe 85 wa ndugu Athanas Lenge Seni tarehe 30 Aprili, 2023 zikiwa katika Kijiji cha Mwamapuli Mkoa wa Katavi na kuingizwa hifadhini ambapo hadi sasa bado wanashikiliwa hifadhini.

6. Viambatisho vingine alivyowasilisha kwa ajili ya kurahisisha rejea ni pamoja na mchango wake wa maandishi alioutoa hapa Bungeni kuhusu jambo hili, Maelekezo ya Waziri Mkuu kuhusu jambo hili aliyoyatoa Bungeni tarehe 27 Aprili, 2023 pamoja na Kanuni za *Animal Welfare* za Mwaka 2020.

**Waheshimiwa Wabunge,** kwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Wazri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) alisimama chini Kanuni ya 75 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 "*Kuhusu Utaratibu*" ambapo alilieleza Bunge kuwa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) alivunja Kanuni ya 71(1)(a) ambayo inakataza Mbunge kutoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

**Na kwa kuwa,** vielelezo vya ushahidi vilivyowasilishwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb), vinaashiria upo upuuzaji wa maagizo ya Waziri Mkuu ya tarehe 27 Aprili, 2023 kuhusu kukomeshwa kwa operesheni za kukamata wafugaji, nimeridhika na uthibitisho wa vielelezo hivyo na kwamba licha ya maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu bado operesheni hizo zinaendelea kufanyika.

**Waheshimiwa Wabunge,** kwa kuzingatia maelezo hayo, mwongozo wangu katika jambo hili ni kwamba mchango wa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) ulikuwa sahihi na hakuna sehemu

aliyovunja Kanuni ya 71(1)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kama ilivyoombwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu).

Aidha, pamoja na vitendo hivyo ambavyo vinaashira kuwepo na kuendelea kufanyika, wote tunatambua mchango wa Mhe. Waziri Mkuu katika kushughulikia jambo hili ambapo ameendelea kusisitiza kila siku hatua za haraka kuchukuliwa katika kuleta mahusiano mema kati ya maeneo ya Uhifadhi na Wananchi. Kwa sababu hiyo, naelekeza maneno ya Mhe. Mpina kwamba "*Waziri Mkuu mwenyewe anaruhusu haya mambo yafanyike na yanafanyika kwa ridhaa yake*" yaondolewe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Dkt. Tulia Ackson (Mb)
**SPIKA**

10 Mei, 2023

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, pia katika Bunge hili mtakumbuka alichangia Mheshimiwa Aida Khenani hapa Bungeni na nikawa nimemuagiza kwamba alete vielelezo kwa sababu tuhuma zilizokuwa zimetolewa zilikuwa nzito kidogo kuhusu Mfuko wa *TASAF* na Mheshimiwa Aida kama alivyotakiwa alileta na yeye vielelezo vyake ofisini, tukapata nafasi ya kupitia Taarifa Rasmi za Bunge na mchango wake aliokuwa ameutoa na zile tuhuma zilizokuwa zimetolewa, lakini pia tulipata nafasi ya kupata vilelezo upande wake na upande wa Serikali kwa maana ya Serikali Kuu, lakini pia tulipata vielelezo kutoka upande wa Serikali kule kutoka Mkoa wa Katavi.

Kwa ujumla wake yale ambayo Mheshimiwa Aida alikuwa ameyaeleeza hapa ndani kuhusu upendeleo wa watu kupewa ule usaidizi ambao Serikali inatoa kupitia Mfuko wa *TASAF,* lakini upendeleo kwa maana ya kichama kwa vyama vya upinzani kuna mazingira kidogo wanakuwa wanakosa huduma hiyo halafu

wengine wanaipata na kwamba wale waliokuwa wanapata wengine wameondolewa kwenye ule utaratibu na mambo kama hayo kwa hiyo aliyazungumza mengi na huu mwongozo pia utaingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge lakini maamuzi ya jumla ni kwamba tuhuma zile alizokuwa amezitoa Mheshimiwa Aida hapa Bungeni hazikuwa na ukweli. *(Makofi)*

## MAELEZO YA SPIKA KUHUSU MALALAMIKO YALIYOWASILISHWA NA MHE. AIDA JOSEPH KHENANI JUU YA WANANCHI WA JIMBO LAKE KUONDOLEWA KWENYE ORODHA YA WANUFAIKA WA TASAF KWA SABABU ZA KISIASA NA MALALAMIKO KUHUSU KITENDO CHA MKUU WA MKOA WA RUKWA NA MKUU WA WILAYA YA NKASI KUTOA KATAZO KWA WATUMISHI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI KUMPA USHIRIKIANO – KAMA YALIVYOANDALIWA

---

**Waheshimiwa Wabunge,** mtakumbuka kwamba tarehe 20 Aprili, 2023 wakati Mhe. Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini akichangia mjadala wa Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) alitoa Malalamiko Bungeni kuhusu Masuala makuu mawili yafuatayo:-

(a) Kwamba wapo wananchi wa Jimbo la Nkasi Kaskazini ambao ni Wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wameondolewa kwenye Orodha ya Wanufaika wa TASAF kutokana na itikadi za Kisiasa; na

(b) Kwamba Mkuu wa Mkoa wa Rukwa na Mkuu wa Wilaya ya Nkasi wametoa katazo kwa Watumishi wa Serikali katika Halmashauri hiyo kutompa ushirikiano wowote kwa vile yeye ni Mbunge wa Upinzani (CHADEMA).

**Waheshimiwa Wabunge,** kwa kuzingatia uzito wa Tuhuma hizo, nilitoa Maelekezo kwa Mhe. Aida Joseph Khenani kuniletea ushahidi wa madai yake, kwa kuwasilisha majina ya Wananchi ambao ni wanachama wa CHADEMA walioondolewa kwenye Orodha ya Wanufaika wa TASAF ili hatimaye Bunge liweze kuchukua hatua.

Aidha, nilimtaka Mhe. Aida Joseph Khenani aniletee mrejesho na ushahidi wa yeye kubaguliwa na Viongozi aliowataja.

**Waheshimiwa Wabunge,** kufuatia maelekezo hayo, tarehe 25 Aprili, 2023 nilipokea barua kutoa kwa Mhe. Aida Joseph Khenani akiwasilisha vielelezo na ushahidi wake kuhusu malalamiko tajwa hapo juu. Vielelezo alivyowasilisha ni pamoja na Orodha ya wananchi wanaodaiwa kuwa ni Wanachama wa CHADEMA na wakaondolewa kwenye orodha ya Wanufaika wa TASAF, stakabadhi mbalimbali za malipo na marejesho ya TASAF na Barua kadhaa alizowahi kuandika kwa Viongozi kuhusiana na malalamiko yake kwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa na Mkuu wa Wilaya ya Nkasi kutoa katazo la yeye kutopewa ushirikiano.

**Waheshimiwa Wabunge,** baada ya kupokea na kuzingatia barua za Mhe. Aida Joseph Khenani na viambatisho vyake, tarehe 11 Mei, 2023 nilifanya mazungumzo na Mhe. Waziri Mkuu na baadaye kufanya Kikao cha pamoja kati ya Mbunge na Mawaziri wanaohusika na sekta zinazolalamikiwa ili kupata uelewa wa pamoja na kutafuta namna bora ya kushughulikia malalamiko ya Mbunge na ili pia niweze kutoa uamuzi Bungeni kuhusu masuala hayo.

Kwa kuzingatia vikao hivyo, napenda kutoa maelezo kuhusu masuala haya mawili yaliyowasilishwa na Mhe. Aida Joseph Khenani kama ifuatavyo:-

(a) Kuhusu wananchi wa Jimbo la Nkasi Kaskazini ambao ni wanachama wa CHADEMA kuondolewa kwenye Orodha ya wanufaika wa TASAF kwa itikadi za kisiasa; Maelezo ya Waziri husika na Wataalam wa TASAF yamethibitisha kuwa zoezi la kuwaondoa watu kwenye Orodha ya Wanufaika wa TASAF lilizingatia vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria na Taratibu. Hivyo wananchi walioondolewa ni wengi zaidi ya wale wa CHADEMA waliotajwa na Mbunge. Aidha, tathmini zaidi ya madai ya Mbunge inaonyesha kwamba: -

(i) Hakuna wananchi walionyimwa fursa ya kupata Fedha za TASAF kwa itikadi za Kisiasa, isipokuwa baadhi ya majina yaliyowasilishwa na Mbunge hayamo kwenye Fomu na Orodha maalum zinazotumika na TASAF na wengine hawakukidhi vigezo stahiki;

(ii) Hakuna wananchi wafaidika walioondolewa kwenye Orodha isipokuwa wale wasiostahili kwa kuzingatia taratibu zilizopo. Aidha, watu 4 kati ya 18 waliodaiwa kuondolewa kwenye Orodha ilithibitika kwamba wamo na wanafaidika; na

(iii) Madai kuhusu waliokuwa wanalipwa kuondolewa na kutakiwa kulipa fedha walizochukua yanatokana na uhakiki uliofanyika kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na sio itikadi za vyama. Kwa mfano katika zoezi la uhakiki wananchi wasio na vigezo wapatao 312 waliondolewa kwenye mpango wa TASAF Wilayani Nkasi.

**Waheshimiwa Wabunge,** kwa kuzingatia maelezo hayo ni wazi kwamba zoezi la kubaini wanufaika wa TASAF linahusisha mchakato usiotawaliwa na itikadi za vyama, ubaguzi wa rangi, sura wala dini ya mtu.

(b) Kuhusu suala la Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kukataza Watumishi wa Halmashauri ya Nkasi kushirikiana na Mbunge; Haikuweza kuthibitika bayana kwamba katazo hilo lilitolewa, bali ilidhihirika kwamba kumekuwa na Changamoto ya kimahusiano kati ya Mbunge na Viongozi wenzake. Kwa kuzingatia hilo, Kikao kilitoa rai kwa Mbunge kuendelea kutambua mchango wa Serikali katika kufanikisha miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa Jimboni kwake, kuendelea na kazi ya kuwatumikia watu wake huku akichukua hatua za kujenga ushirikiano mwema na kuaminiana miongoni mwa wadau mbalimbali wa maendeleo kwenye Jimbo Lake.

**Waheshimiwa Wabunge,** nitumie fursa hii kutoa rai kwa Wabunge wote kuendelea kudumisha mahusiano mazuri na Viongozi na Watumishi waliopo katika maeneo yetu. Sambamba na hilo,

Viongozi na Watumishi wa Serikali waliopo kwenye maeneo mbalimbali wanapaswa kutoa ushirikiano kwa Waheshimiwa Wabunge ili wote kwa Pamoja waweze kuwatumikia vizuri wananchi.

**Waheshimiwa Wabunge,** kwa maelezo hayo sasa nazifunga rasmi hoja zilizowasilishwa kwangu na Mhe. Aida Joseph Khenani tarehe 20 Aprili, 2023 wakati akichangia Bungeni.

Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Mb.
**SPIKA**

15 Mei, 2023

**SPIKA:** Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tutakuwa hatuna jambo ambalo lilikuwa limejitokeza hapa ambalo lilikuwa linahitaji Kiti kitoe mwongozo ama kieleze kuhusu utaratibu ambalo litakuwa limesalia na kwa hivyo tutakuwa na sisi tumemaliza yale yote yaliyokuwa yanayahusu Bunge hili.

Waheshimiwa Wabunge, ametutajia hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe ya kurejea hapa Bungeni na kwa hivyo na mimi nitumie fursa hii baada ya shukrani hizo kwa watu wote, nitumie fursa hii sasa kuahirisha Shughuli za Bunge mpaka tarehe aliyoitaja Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ni taerehe 29 Agosti, 2023 saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 5.50 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 29 Agosti, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*